

KUTAMBUA SIKU YAKO

NA UJUMBE WAKE



Habari za asubuhi, wapendwa. Hebu na tuendeleo kusimama kwa muda kidogo tu.

Mungu mpendwa, sisi, tulio kwenye wakati wa mahangaiko na kakara za maisha, tumetulia kwa dakika hizi chache zifuatazo ama kwa saa, chochote kile, ambacho Wewe umetujalia, ili tukusifu na kukutukuza, kuhubiri Neno Lako, kukujua vyema zaidi, hiyo ndiyo sababu tumekusanyika asubuhi ya leo. Tunakushukuru, Mungu, kwa sababu kuna watu ambao wako tayari na wamejiandaa kuja kusikiliza. Pasipo kujali hali na wakati, na ambao tunaishi, wangali wanaamini. Nasi tunakushukuru kwa ajili yao.

² Mungu, tunakushukuru kwa ajili ya nguvu Zako kuu za kuponya, ahadi za Neno Lako. Jinsi mioyo yetu inavyowaka moto tunaposikiliza shuhuda hizi! Kila namna ya mateso ambayo yameletwa juu ya wana wa Adamu! Wewe, na neema Yako na nguvu, na pamoja na ahadi Yako, umewaponya. Nao wako hapa, wakishuhudia, wakimpa Mungu sifa. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili.

Na sasa twaomba, leo, tusikie Ujumbe ambao umetuandalia kwa ajili ya saa hii. Tunaposoma katika Neno Lako, tunaomba utupe ufahamu wa yale tunayosoma. Mapenzi Yako na yatendeke katika mambo yote, kwa kuwa tunayaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaweza kuketi.

³ Ni majaliwa kuwa hapa asubuhi ya leo. Nina furaha sana kwa ajili yenu ninyi nyote. Na ndugu Woods, Ndugu Roy Roberson, ndugu wengine wengi, wamefanya kazi kwa uaminifu siku mbili zilizopita, kuyoyozi jengo hili kwa kusudi hili, maana Jumapili iliyopita waliona jinsi mlivyoteseka. Nao walikuwa na pesa kidogo katika hazina ya kanisa, nao wakaingia kazini na kuvifungulia viyoyozi hivyo mpate kujisikia vizuri, kwa pesa mlizotoa kwenye sadaka, ambapo mnaweza kuketi, kusikiliza Ujumbe. Kumepoa zaidi leo kuliko ilivyokuwa hapo kabla. Kwa hiyo tuna shukurani kwa Mungu, na kwenu ninyi watu, kwa ajili ya fursa hii.

⁴ Nafurahi. . . Ndugu Roy Borders, yeye alitaka kwa namna fulani kuketi huko nyuma asubuhi ya leo. Nami nilimwambia achukue kiti chake na kuketi hapa pamoja na wahudumu hawa, bali hakupenda kufanya hivyo. Kama ninyi nyote mjuavyo, Ndugu Borders anatuwakilisha hudumani. Nina furaha sana

kuwa na Ndugu Borders hapa, na wahudumu wengine wengi pamoja na marafiki.

⁵ Juma hili lote ni—nimekuwa nikifikiri, na kusema, “Nitakapofika huko, Jumapili, nitamsalimia kila mhadumu, kila mtu.” Ndipo unapofika hapa, unachukuliwa sana na Ujumbe mpaka unasahau tu kila kitu, karibu kila kitu, kwamba kilikuwa ni kitu gani.

⁶ Sasa inanibidi nirudi Arizona. Sina budi kurudi Jumatatu ijayo, juma lijalo, kurudi Tucson, kuwapeleka watoto huko wakasome. Ndipo nitarudi tena basi baada ya hapo. Na inabidi mke wangu awahi huko, kuanza ninii . . . kuwaandikisha watoto, majuma mawili kabla ya shule kuanza. Na mimi, basi, nitarudi nikae kwa muda kidogo hapa.

⁷ Na sasa huu ni wakati wangu wa likizo. Kama mjuavyo, nimehubiri tangu Desemba; Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei, Juni, na Julai. Sasa, Mungu akipenda, na kusiwe na wito wowote maalum, huu ndio msimu ambao mimi—mimi—mimi hupumzika, likizo yangu. Ninaenda kuwinda. Nami . . .

⁸ Sasa kama Bwana akiniitia jambo lingine, mambo hayo hayako kwenye picha tena. Mungu daima ni wa kwanza. Nami ninataka awe wa kwanza, nanyi mnataka Yeye awe ni wa kwanza. Lakini basi kama hakuna wito dhahiri, na hayo yawe ni mapenzi Yake, hivyo ndivyo nitakavyopaswa kufanya sasa kwa miezi michache ijayo, ni kwenda kuwinda sasa, nipate kujipumzisha. Mimi . . .

⁹ Hamtambui, ulimwengu hautajua kamwe, mambo yanipasayo kupitia. Unaona? Na ni uchovu mwingi sana wa akili. Si ajabu Bwana aliwaambia wanafunzi Wake, wakati alipokuwa akitembea pamoja nao, “Njoni huku jangwani, mpate kupumzika kidogo.” Unaona? Ninatambua jambo hilo zaidi, kila siku, na zaidi sana kadiri siku zangu zinavyozidi kuongezeka duniani, unaona. Kadiri ninavyozidi kuwa mzee, mtu unatambua jambo hilo. Mnamsikia mchungaji wetu akisema “amina” kwa jambo hilo, pia. Yeye, sisi, tunaweza kutambua ya kwamba sisi si vijana baada ya kupita umri wa miaka hamsini. Sasa hatuna budi kuwa na wakati kidogo.

¹⁰ Tunashukuru sana kwa ajili ya shuhuda ambazo tumesikia sasa hivi. Mke wangu alikuwa huko kwa Bibi Wood, jana, wakati watu fulani walipokuja kutoka Alabama, sehemu fulani kule, nao walikuwa wakisimulia habari za mambo makuu aliyofanya Bwana katika mkutano huo, habari za kuponywa kwa watoto wadogo, na mambo mbalimbali. Na mambo mengi sana ambayo, jamani, ingechukua muda mrefu sana ku—kuyasimulia.

¹¹ Tena mimi pia sina budi kukumbuka ya kwamba . . . ninaamini baadhi yao waliniambia ya kwamba Dada Larson amekuwa hapa Jumapili mbili akiwa na mtoto mchanga. Nisingejua, lakini ninaamini walisema ilikuwa ni mjukuu wake,

labda, kwa ajili ya kuwekwa wakfu, akimleta kutoka Chicago. Bibi huyo amekuwa mkarimu sana kwetu, nasi tunamthamini. Naye alimleta mtoto mchanga kutoka Chicago, kwa ajili ya kuwekwa wakfu. Ambapo, ana muda mfupi sana wa kumtoa, nafikiri, kwa ajili ya kuwekwa wakfu, lakini anataka sana mtoto huyu awekwe wakfu kwa Bwana. Kwa hiyo kama Dada Larson akiweza, wakati nikiwa ninazungumza, naomba amlete tu mtoto huyo mchanga kwa ajili ya ibada hii ya kuwekwa wakfu.

¹² Na halafu, pengine, wakati akijitayarisha, ni—ninataka kusema kwamba huu umekuwa ni Ujumbe mgumu sana nilipata kujaribu kutayarisha, mpaka jana usiku. Juma zima, ningeingia chumbani, kujaribu kuketi faraghani baada ya kupokea simu zangu na kadhalika, ku—kujaribu kupata kitu fulani mawazoni mwangu kwa ajili ya wakati huu. Na wakati ningeenda, ni—nisingeweza hata kuninii... Kichwa changu kilikuwa kitupu. Na, jana, niliingia kwenye orofa ya chini ya ardhi. Nilifikiri kulikuwa na joto sana, kwa hiyo nikashuka kwenda kwenye orofa ya chini ya ardhi, nikaketi huko. Nami ningejaribu kuchukua Biblia yangu na kuisoma, na ningesikwa na usingizi. Ndipo ningeamka na kunywa maji, na kujaribu kujitikisa, halafu nitoke nje na kuzunguka, niketi kwenye kipandio.

¹³ Mtu fulani alipitia pale akanikuta nimevua shati langu, nimeketi kwenye kipandio; kulikuwa na joto sana. Wakanipungia mikono. Sikujua kama walinipungia mikono... Mtu fulani, huenda ilikuwa ni mtu fulani hapa mjini, ama huenda ilikuwa ni mtu fulani hapa kanisani, aliyenipungia mikono. Na—nami nilikuwa nikiwaza tu, ilitokea tu kwamba ni—nililitupia jicho hilo gari, lililopita. Nikampungia mkono.

¹⁴ Jana jioni niliingia kwenye gari nikaenda nikielekea huko Charlestown, nikijaribu kupata kitu fulani. Bwana, ilionekana kana kwamba, alitaka kuniambia jambo fulani, lakini mimi... Shetani alikuwa akijaribu kunizuia, kunizuia kufanya jambo hilo. Kwa hiyo nikawazia, "Vema, kama anafanya hivyo, nitaendelea tu kungoja, niendelea tu kungoja, nikibisha mlango kwa nguvu mpaka Yeye atakapofungua." Kwa hiyo basi muda kidogo tu uliopita, ama karibu tu kwenye saa moja asubuhi ya leo, nilikuwa nimeamka mapema sana.

¹⁵ Jana, nilikuwa mgonjwa kidogo, nikijaribu... Nilikuwa nimekula mahindi ambayo hayakupatana nami sawa sawa, kwa kuwa yalikuwa makali sana, nami ni—nilikuwa nikijaribu kuachana nayo. Na—na basi asubuhi ya leo, kwenye saa mbili, ilitokea kwamba nilichukua Andiko ambalo lilinishangaza sana. Ndipo nikaangalia Andiko hilo tena, na tena likanishangaza sana. Ndipo nikaenda, nikilifuatilia kwenye Maandiko, na ndio kwanza nimalize tu dakika chache zilizopita. Kwa hiyo huenda ikawa Bwana ana Ujumbe kwa ajili yetu, asubuhi ya leo, ambao Shetani amejaribu kutuzuia tusiupate.

Unaweza kumleta huyo mtoto hapa, Dada Larson? [Ndugu Branham anamweka mtoto wakfu. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mungu awe pamoja nao na awasaidie.

¹⁶ Sasa nimekuwa nikiwachelewesha, Jumapili iliyopita, siku mbili, nami ninafikiri. . . ama, ibada mbili, asubuhi na jioni, na hilo linakuwa ni gumu kwenu. Nasikia ya kwamba. . . Wengine wenu inawabidi kusafiri mbali sana, na kukosa kazi siku moja, na kadhalika. Kwa hiyo hata kama tutaondoka Jumapili, Jumatatu, juma moja, nitatangaza tu ibada ya Jumapili ijayo, Bwana akipenda, unaona, isipokuwa kusanyiko liwe linataka kukaa usiku huo. Unaona, hilo, hilo ni juu. . . Mko wengi sana!

Ni wangapi wangependa kwamba iwe ni usiku wa leo, hebu tuone, kwamba tuwe na ibada usiku wa leo? Sasa, anayetaka tuifanye Jumapili ijayo, inua mkono wako pia? Jamani, karibu wako sawa. Loo! [Mtu fulani anasema, “Tumeenda sare, ndugu!”—Mh.] Wasemaje? [“Tuifanye nyakati zote mbili.”] Loo! [Ndugu Ben Bryant anasema, “Na, usiku wa leo, tuwe na ibada mbili.”] Sasa, sasa, Ben! [Ndugu Branham anacheke.]

¹⁷ Nina Ujumbe huu, ni mrefu, asubuhi ya leo, lakini si—sijui ni vipi tu. . . Nami ninajua ninasaidia kuweka sheria za kanisa, lakini kuhusiana na hilo, kama mtakumbuka, nilisema, “Isipokuwa niwe ninarekodi.” Unaona? Kwa hiyo, huu ni wa kurekodiwa. A-ha. Kwa hiyo labda tutajaribu kurudi mara hizo mbili, usiku wa leo na Jumapili ijayo, basi, tutafanya hivyo Bwana akipenda, unaona. Sasa, kama usipopata ujumbe juma hili, basi njoo Jumapili ijayo.

¹⁸ Ninachukia kuwafanya mje mara mbili namna hiyo, lakini ninajisikia hatuna ila muda mdogo tu zaidi. Na hebu kumbukeni tu, kama wakati ukiendelea, hatutakuwa na majaliwa haya kwa muda mrefu sana. Unaona? Kumbukeni, jambo fulani litatukia. Ama sheria itatukataza, ama Shetani ataingia miongoni mweni na kuwatawanya. Imekuwa hivyo daima. Unaona? Jambo fulani litatukia, kwa hiyo hebu na tuithamini kila dakika tunapokuwa pamoja.

¹⁹ Kwa hiyo sasa kwa wale ambao inabidi mrudi kwenye makazi yenu, usiku wa leo, itakuwa kama usiku wa Jumapili iliyopita, nilikuwa tu na Ujumbe m—mdogo mfupi. Na kwa hiyo, wewe, kama unataka kwenye kanda, mbona, bila shaka tutakupelekea kanda hiyo kama inakubidi kurudi nyumbani. Sisi hatu-. . . Nitahubiri usiku wa leo, Bwana akipenda.

²⁰ Nilikuwa na muhtasari jana, ama—ama juzi, Ujumbe mdogo nilioandika kutoka kwenye kumbukumbu la jambo fulani, na ni wa siku nyingi. Kuna Jumbe mbili, hata hivyo. Kwa namna fulani uko katikati, mmoja wao ni, “Birika linalovuja,” au ama, “Kupanda upepo na kuvuna kimbunga,” Ujumbe tu wa Injili. Asubuhi ya leo ni kufundisha. Na kwa hiyo, usiku

huu, nitazungumza aidha juu ya, “Kupanda upepo na kuvuna kimbunga,” ama, “Birika ambalo linavuja.”

²¹ Na, asubuhi ya leo, ninataka kusoma kutoka katika Maandiko Matakatifu sasa.

Na je! mmestarehe? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.—Mh.] Vema.

Sasa ninawatakeni, katika Biblia zenu, mfungue pamoja nami kwenye Kitabu cha Hosea, ninyi mnaopenda kusoma. Na hebu tusome vifungu vichache kutoka kwenye mlango wa 6 wa Kitabu cha Hosea, yule nabii.

Na hebu na tusimame.

²² Mungu mpendwa, hatustahili kukitwaa Kitabu hiki mikononi mwetu, kwa kuwa tunasoma katika Maandiko ya kwamba hakuna mtu Mbinguni wala duniani, wala chini ya nchi, aliyestahili ama hata aliyeweza kukitwaa Kitabu hiki, wala hata kukitazama. Loo, ndipo akaja Mmoja ambaye alikuwa kama mwana-kondoo aliyechinjwa; akakitwaa hicho Kitabu, kwa kuwa Yeye alistahili, ndipo akafungua hiyo Mihuri. Nasi tunamtegemea Yeye asubuhi ya leo kufunua maneno haya ya utangulizi yaliyoandikwa katika Kitabu hiki, kwa maana ni Kitabu cha Ukombozi. Wote waliokombolewa wameandikwa mle. Jalia tupate nafasi yetu, asubuhi ya leo, katika wakati tunaishi. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Njoni sasa, tumrudie BWANA; maana yeye amerarua, na yeye atatuponya; yeye amepiga, na yeye atatufunga jeraha zetu.

Baada ya siku mbili atatupokea; siku ya tatu atatuinua, nasi tutaishi mbele zake.

Nasi na tujue, naam, tukaendele kumjua BWANA; kutokea kwake ni yakini kama asubuhi; naye atatujilia kama mvua, kama mvua ya masika na mvua ya vuli iinyweshayo nchi.

Ee Efraimu, nikutendee nini? Ee Yuda, nikutendee nini? Kwa maana fadhili zenu ni kama wingu la asubuhi na kama umande utowekao mapema.

Kwa sababu hiyo nimewakata-kata kwa vinywa vya manabii; nimewaua kwa maneno ya kinywa changu; na hukumu yangu itatokea kama mwanga.

Maana nataka fadhili wala si sadaka; na kumjua Mungu kuliko sadaka za kuteketezwa.

Lakini wao wamelivunja hilo agano kama Adamu; huko wao—wao wamenitenda mambo ya hiana.

Gileadi ni mji wa hao watendao maovu, umetiwa rangi ya damu.

Na kama vile makundi ya wanyang'anyi wamwoteavyo mtu, ndivyo kundi la makuhani wauavyo katika njia ielekeayo...na...wametenda mambo maovu sana.

Katika nyumba ya Israeli nimeona jambo bovu kabisa; huko uzinzi umeonekana katika Efraimu; Israeli ametiwa unajisi.

Tena, Ee Yuda, wewe umeandikiwa mavuno, hapo nitakapowarudisha wafungwa wa watu wangu.

²³ Bwana Yesu, twaa kutoka kwenye Hili, kwa Roho Wako Mtakatifu, somo linalokusudiwa, tunapoendelea kukungojea Wewe. Katika Jina la Yesu. Amina.

²⁴ Sasa, somo langu asubuhi ya leo ni: *Kutambua Siku Yako Na Ujumbe Wake.*

Tunaona kutoka kwenye somo la Jumapili iliyopita, tulipokuwa tukifundisha, *Sikukuu ya Baragumu*. Nami nataka mnisikilize vizuri, sasa, majira—majira ya Israeli katika saa ya Mungu.

²⁵ Tunashughulika leo na somo la shule ya Jumapili, kwamba ninawataka mtambue na kujua wakati tunaishi. Tuko karibu sana na kufikia mwisho, kama mnavyoon. Halafu basi, kwa jambo hili, mnapaswa kujua kabisa saa yenyewe na wakati, na ishara na Ujumbe ambao mnapaswa kuupokea.

²⁶ Sasa, kama tulivyoanza Jumapili iliyopita...Tulikuwa tukizungumza juu ya kwenda kuhubiri juu ya zile Baragumu, zile Baragumu Saba za mwisho za Biblia. Na mimi, moyoni mwangu, nilifikiri zingetokea tu kama ile Mihuri. Lakini nimeona kwenye kila moja ya huku kufunguliwa kumekuwa na jambo la ajabu sana lililotukia.

Na kama ambavyo tulihubiri juu ya *Nyakati Saba za Kanisa*, nazo zilikuwa ni kamilifu sana mpaka Roho Mtakatifu Mwenyewe akashuka miongoni mwetu na kuthibitisha jambo hilo, na likawekwa kwenye magazeti, na kulisambaza nchini kote, na kulionyesha kwenye mwezi mbinguni, na kulithibitisha kwetu, majuma na miezi kabla halijatukia, kwamba hivyo ndivyo ingetukia hasa, kikamilifu. Yeye alitujulisha jambo hilo hapa Maskanini. Hapa kwenye...katika wakati ule, Yeye alilijulisha. Kwenye mwezi na jua, alilitambulisha. Na katika hali ya mataifa ilivyo kwenye wakati huu, Yeye alilitambulisha; wakati kiongozi wa ukasisi wa Rumi alipoondoka na akarudi Palestina ikiaminiwa alikuwa ndiye papa wa kwanza aliyerudi kule tangu (wao wanadai) Petro akiwa ndiye papa. Sasa, ilikuwa ni ajabu sana!

²⁷ Halafu, tunaona, kabla ya zile Mihuri Saba ambayo ilificha siri zote.

Mimi bila kujua nilichokuwa ninachora ubaoni, kwa ajili ya Nyakati za Kanisa. Sikujua kamwe. Mungu anajua. Ni kwa ono tu, nilichora. Bila kujua ya kwamba Mungu, mwaka mmoja na miezi sita baadaye, angethibitisha jambo hilo mbinguni, kwa mwezi, na kuliingiza kwenye magazeti ya taifa. Mimi sikujua jambo hilo. Sikujua kungekuwa na giza totoro la ajabu mwezini, kuwakilisha Wakati huu wa Laodikia.

²⁸ Sasa, kwenye magazeti, unapata nyakati sita tu. Ni kwa sababu kanisa la Laodikia liliingia giza kabisa. Na kama mngeweza kuona matumizi ya kiroho, kama vile Mungu alivyoyaweka huko mbinguni. Wakati nilipoyaweka hapa duniani, niliacha nafasi ndogo sana, kama mnavyoona, nuru kidogo mno. Hiyo ilikuwa ni kabla tu ya Wateule kuitwa kutoka duniani, ndiyo sababu niliweka pale kwa ajili ya wakati wa saba. Bali wakati Mungu alipoiweka huko mbinguni, ilikuwa ni giza tupu, inamaanisha labda yule wa mwisho ameitwa kutoka kwenye Wakati wa Laodikia. Hatujui. Kungeweza kuweco na mahubiri juu ya jambo hilo.

²⁹ Sasa angalia tena, kabla ya ile—ile Mihuri Saba, ambayo sikuwa na fununu ilikuwa hivyo.

Hapa Maskanini Yeye alinena juu ya jambo hilo, na akanituma huko Tucson, Arizona, nikiwaambia ninyi nyote ambayo yangetukia. Na yupo mtu hapa aliyeketi, leo, aliyekuwa kule kuliona likitukia jinsi hasa ilivyosemwa hapa lingetukia, “Malaika saba wangekuja.” Ndipo magazeti yakaandika jambo hilo, na majarida, kote nchini, “Duara ya Nuru ya ajabu katika umbo la piramidi,” kama tu vile nilivyoichora hapa na kuwaonyesha ninyi. Iliinuka kutoka mahali ambapo hao Malaika walikuwa wamesimama, na ikapanda juu maili thelethini, na ilikuwa maili ishirini na saba kutoka upande mmoja hadi mwingine; ama aidha maili ishirini na saba kwenda juu, na maili thelathini kutoka upande mmoja hadi mwingine, ninasahau ilivyokuwa. Na ilionekana kote mikoani, juu kidogo tu ya Tucson, Arizona, mahali pale pale ilipotukia, wakati ule ule.

³⁰ Unaona, Bi—Biblia, Mungu si ninii tu. . . Hii si mtu fulani anayejaribu tu ku—kusukumiza jambo fulani kwenu, ila ni kuwafunulia matumizi ya kiroho ya saa hii hasa.

³¹ Halafu basi, Ujumbe uliofuata, uliofungua ile Mihuri Saba, ambayo ilifunua siri zote zilizofichwa za Biblia, Mafundisho, na kadhalika. Ambayo, ulimwengu unayapinga kwa ujeuri sana siku hizi, unaupinga Huo na kusema ni wa uongo, *hivi, vile*.

³² Hapa hivi majuzi huko Arizona, walikuwa wanakata na kuziunga kanda, wakijaribu kunifanya niseme mambo ambayo sikuyasema. Kumbukeni tu lile ono kuhusu lile suala la Arizona! Biblia ilisema, “Tlikuwa ni heri sana kwako kwamba ufungiwe mwamba shingoni mwako.” Na jambo lingine,

kwamba, “Mtu yeyote,” acha awe mhubiri ama ye yote yule, “atakayeondoa Neno moja Kwake, ama kuongeza neno moja Kwake!” Watu wakiweka tafsiri yao wenyewe kwenye Neno jinsi lilivyotolewa, wakijaribu kulifanya liseme jambo fulani ambalo mimi sikusema, na, si Neno langu; ni Neno Lake. “Mtu yeyote atakayeongeza, au kuondoa!”

³³ Halafu basi, katika ono hilo, tuliwaona hawa manabii wakishuka chini, kama nilivyowaelezea, ninaamini, Jumapili kadhaa zilizopita. Yote yatatukia. Nikasema, “Msikaribie jambo hilo kamwe.” Mradi tu ninalipiga vita, basi Mungu hawezi kulipiga vita. Bali hebu na tumwache aliingilie. Yeye Ndiye anayelishughulikia. Unaona?

³⁴ Sasa tuliona, Jumapili iliyopita, kulikuwa na... kuhubiri zile siku za sikukuuu. Na kulikuwa na sikukuu ya pentekoste. Na kati ya sikukuu ya pentekoste na sikukuu ya baragumu, hicho kilikuwa ni kipindi kirefu cha wakati; siku hamsini kamili kati ya pentekoste na sikukuu ya baragumu. Na siku hamsini, ambazo, *pentekoste* inamaanisha “hamsini.” Ilikuwa ni kutikiswa kwa mganda, ama ninii... Malimbuko ya mavuno yaliyoletwa. Na tunaona ilikuwa ni katika mfano wa huko nyuma, pamoja na malimbuko ya kwanza kimaumbile, yakiwakilisha malimbuko ya Roho Mtakatifu atakayemwagwa juu ya watu.

Nasi tunaona, basi, ya kwamba zile siku hamsini zilipokelewa na Mataifa, ambapo, “Mungu aliita kutoka kwa Mataifa watu kwa ajili ya Jina Lake,” sikukuu ya pentekoste. Nasi tumekuwa tukipitia sikukuu hiyo kubwa ya pentekoste.

³⁵ Sasa, kwa kweli, kutoka kwenye hizo siku hamsini, ingekuwa ni Sabato saba kamili. Na Sabato saba ziliwakilisha Nyakati Saba za Kanisa, zitakazoitwa katika wakati wa sikukuu ya kipentekoste, ya Pentekoste, kuwaita watu kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake.

Sasa, katika mwisho wa hizi Sabato saba, ambazo zimekuwako, kulikuwa kuwe na Sikukuu ya Upatanisho, ambayo ilikuwa ni zile Baragumu Saba. Na zile Baragumu Saba zilikuwa za kutangaza siku ya maombolezo, kurudi kwenye ile Dhabihu, ama, ule Upatanisho. Nasi tunaona ya kwamba basi, ya kwamba, Israeli, zile Baragumu Saba ziliwahusu tu Israeli.

³⁶ Na, basi, sababu ya Yeye kunikataza kuhubiri hizo Baragumu Saba. Hata nilikuwa tayari kutangaza jambo hilo, nilikuwa nimeandaa kumbi za mikutano na kila kitu tupate kwenda huko, kuhubiri zile Baragumu Saba. Ndipo nikasema, “Kuna jambo fulani linalonisumbua sana,” nilisema. Tukaendelea kufanya kazi, na Billy na sisi wote, tukijaribu kuandaa kila kitu tayari kwa ajili ya hilo jengo lililo na viyoyozi, kwa ajili ya juma hilo lijalo, kwa ajili ya zile Baragumu Saba;

tukiwa tuna siku kumi, ama siku nane, tulikuwa na ukumbi wa shule. Bali Roho Mtakatifu asingeniruhusu kufanya jambo hilo, kwa sababu fulani, nami nikashangaa ni kwa nini.

Na nilipoenda kuomba, nilimwambia mke wangu, “Naenda kujifungia.” Na kwa uaminifu nikapiga magoti mbele za Mungu, kuomba. Ndipo akanifunulia ya kwamba hizo Baragumu Saba zilitoa sauti zao chini ya Muhuri wa Sita, nami tayari nimekwisha kuzihubiri, kimbinguni. Unaona, ni mkono wa Mungu, jambo hilo lote. Zinahusu Israeli, nasi tulizichukua chini ya ule Muhuri wa Sita; ninyi nyote mlilo nao huo, jinsi ambavyo yale mateso ya Wayahudi.

³⁷ Wakati wa Mataifa umekuwa katika sikukuu hii ya kipentekoste.

Zile Baragumu, chini ya . . . zote zilipigwa chini ya Muhuri wa Sita. Nasi tuliuchukua huo Jumapili iliyopita, chini ya sikukuu ya baragumu, kama nyote mnataka kupata jambo hilo. Zilihusu nini? Kuwatimua Wayahudi, kutoka sehemu zote za ulimwengu, warudi katika nchi ya uenyeji wao. Wanapaswa kuwa kule. Na kule kufunguliwa kwa ile Mihuri, chini ya Muhuri wa Sita, na chini ya . . . Zile Baragumu Saba zilipigwa katika—katika Muhuri wa Sita.

³⁸ Sasa, Ujumbe wa Malaika wa Saba utafungua siri ya ile Mihuri, ikiita wafanya kazi wa saa kumi na moja wa Mataifa wapate ujira ule ule ambao wale wafanya kazi wa saa moja walipata. Unaona?

Sasa, Yesu alifundisha jambo hilo. Alisema kulikuwa na watu walioenda kuvuna. Walikuwa wamekodishwa. Nao walipoenda, alfajiri, walipata wa—wa—wakati, dinari kwa siku. Ndipo alasiri, mtu mwingine aliingia na kuanza kazi. Na halafu saa kumi na moja, hiyo ndiyo saa ya mwisho ya siku, ndipo mtu mmoja alipokuja na akapokea ujira sawa na wengine waliopata alfajiri; saa ya mwisho.

³⁹ Ni kamilifu sana, jinsi ambavyo wajumbe wa alfajiri wakiwa na Neno, wakiwa na Injili, wakiwa na Kweli, walikuja katika Siku ya Pentekoste. Ndipo kulikuwa na wakati wa giza uliowafunika. Ndipo katikati ya mchana, Luther, na Wesley, na hao wengine, wakaingia. Na halafu kutakuwa na Ujumbe wa jioni, na kupokea kitu kile kile walichopokea hapo mwanzo. Ujumbe wa wakati wa jioni ni wa kurejesha, kurudisha kitu kile kile tena.

⁴⁰ Na kumbukeni lile ono la juma lililopita, ambapo Bibi-arusi alikuja kuninii. . . onyesho lake la awali. Alitokea Bibi-arusi mdogo, mzuri, katika lile ono. Na mimi, bila kufikiria jambo hilo; nikiwa nimeketi tu pale nikiangalia nje. Ndipo akaja Bibi-arusi. Nilisikia Sauti kando karibu nami, ikasema, “Hili hapa onyesho la awali la Bibi-arusi.” Naye akapitia pale. Nikamwona, jinsi alivyokuwa, mzuri sana, wa kupendeza,

kijana mbichi. Alikuwa anapiga tu hatua alivyoweza, si mwendo wa kijeshi; ni katika hatua tu za mwa—mwanamke, jinsi wanavyotembea kwa hatua za madaha, kama bibi. Hivyo ndivyo alivyokuwa akitembea, akija kushoto kwangu upande *huu*, kisha akatoweka.

⁴¹ Ndipo Yeye akanigeuza mkono wa kuume, na akanionyesha kila kanisa jinsi ambavyo wametokea kwenye nyakati. Na, loo, ni waovu jinsi gani! Na la mwisho lilikuwa ni la wakati huu wa kanisa la siku ya mwisho, ambalo liliongozwa na mwanamke mchawi. Nao walikuwa wamevaa mavazi ya kiasherati sana, wakionekana wachafu sana! Tena walikuwa wakipiga hatua za kujisokota na za roki. Na hao wanawake wakijitupa katika kukata viuno tu, wakishikilia tu karatasi, ya kijivu, kiunafiki, ninii. . . Kijivu ni kati ya nyeupe na nyeusi, ambayo ni rangi ya udanganyifu. Kijivu si nyeupe wala nyeusi. Ni rangi ya udanganyifu. Na karatasi ya kijivu, wakiishikilia mbele zao, na wamevaa sketi za dansi ya hula wakishikilia mbele zao, na wako uchi wa mnyama kutoka kiunoni kwenda juu. Nao walikuwa wakipiga hatua za. . . ama wakati, ama kujisokota, na kupiga makelele pamoja na muziki huo, wakitembea. Ndipo akasema, “Hilo ndilo kanisa.”

⁴² Na wakati lilipopita karibu nami, moyo wangu nusura uzimie. Nikawazia, “Endapo hilo ndilo linalojaribu kupewa Kristo, kama Bibi-arusi? Kwa jitihada zote na mambo mengine ambayo mwanadamu amefanya, kujaribu kumzaa Bibi-arusi kwa ajili ya Kristo; na ati malaya mshenzi, najisi na mchafu namna hiyo awe Bibi-arusi wa Kristo?” Liliuchefua moyo wangu.

⁴³ Basi alipopita, baada ya yeye. . . Akija mbele ya mahali tulipokuwa tumesimama, alikuwa ameshikilia karatasi mbele yake, akikatika kiuno, na kunengua, na kujisogeza upande mmoja na halafu upande huo mwingine, alipokuwa anaenda, kama dansi la kisasa wanalocheza siku hizi, akijitumia katika tendo kizinzi alipokuwa anatembea kiaskari.

⁴⁴ Mimi sihusiki na mambo haya. Ninaweza tu kusema niliyoona. Na Mungu kama Hakim wangu, bali hilo lilikuwa ni kanisa la kutoka Marekani.

⁴⁵ Sasa, wakati alipokuwa anapita, upande wote wa nyuma haukufunikwa hata kidogo. Na ndipo alipokuwa akipita nilijisikia kuzirai na kuchefukwa.

⁴⁶ Ndipo Yeye akasema, “Bibi-arusi atakuwa na onyesho la awali tena.” Na huyu hapa Bibi-arusi anakuja nyuma yake, Bibi-arusi aliyefanana kabisa na yule aliyepita hapo mwanzoni. Ndipo moyo wangu ukaruka kwa furaha, kujua ya kwamba kutakuwa na Bibi-arusi. Naye atafanyizwa kwa kitu kile kile, na kuvalishwa kitu kile kile, ambacho Yule wa mwanzoni alivalishwa awali. Yeye ataitwa.

Nami ninajua hiyo ni Kweli. Kama hiyo si kweli, basi kila ono ambalo nimeona hapo nyuma limekuwa ni la uongo. Na mtu yeyote anajua, ya kwamba, hakuna hata jambo moja amewahi kutwambia ila lililokuwa ni Kweli. Lilitukia, kama tu . . .

⁴⁷ Na je! mnaweza kuona, basi, ule uchafu wa kanisa la kisasa, linalojiita “kanisa”?

⁴⁸ Kama vile mtu fulani alivyosema hivi majuzi; Ndugu Ruddell, ndugu yangu wa thamani, anayesimama akiegemea ukuta pale sasa. Ya kwamba, yeye aliliona kama kimelea kwenye mzabibu. Nasi tulikuwa tukizungumzia jambo hilo chumbani hivi majuzi. Na Ndugu Ruddell alikuwa anasumbuliwa na hali ya wakati huu na—na kuhisi kwa roho katika makanisa siku hizi, jinsi kumeanza kupungua. Wahudumu wakitoka kila mahali, na usaili unafanyika hapa, wakiuliza, “Ni kitu gani kimetukia, Ndugu Branham? Imekuwaje?” Loo, jamani!

⁴⁹ Ndugu Ruddell aliniuliza swali hilo, “Je! wao wanaishi kwa roho wa Shetani, ama vipi?”

⁵⁰ Nikasema, “La, kimelea kinaishi kwa nguvu za mzabibu.” Kinaishi kwa sababu, tunda chungwa, li—limau litakua katika mchungwa; bali halitazaa machungwa, ingawa linaishi kwa uhai wake.

Na kanisa, linavyojiita, ni kwamba tu ni kimelea kilichopandikizwa, linaishi kwa jina la dini, kwa jina la kanisa. Katoliki na Protestanti, ni vimelea tu, vikinyonya ninii . . . kutoka kwenye nguvu ya Mzabibu; na hata hivyo wakizaa tunda la kile walicho, kwa maana hawakuongoka. Hawakuwa kwenye mpango wa asili uliochaguliwa tangu zamani na Mungu, hiyo ndiyo sababu inabidi walikane Neno na kuzaa tunda la aina nyingine. Mti halisi na wa kweli, katika shina lake, ulichaguliwa tangu zamani kuzaa machungwa kwenye mchungwa.

Yesu alisema, “Mimi ndimi Mzabibu; ninyi ni matawi.”

⁵¹ Lakini kama mti huo ukitoa tawi lingine kamwe, litazaa tunda lake la asili. Na hakuna budi kuwe na kurejeshwa kwa mambo haya yote, moja kwa moja kwenye kilele cha Mzabibu. Inabidi kuwe, kutokee, kurejeshwa, Nuru ya jioni ipate kulimulika na kuliweka sawa. Lakini litatokea kwenye ule Mzabibu, si madhehebu ambayo yamepandikizwa Kwake; bali kuzaliwa asili kwa Neno. Litatokea kwa ajili ya wakati wa jioni. “Na kutakuwako na Nuru wakati wa jioni.” Inahitaji Nuru kuliivisha.

⁵² Angalia jinsi Maandiko yalivyo makamilifu! “Siku ambayo haitaitwa mchana wala usiku.” Tunda haliwezi kuiva lisipoivishwa na jua. Haidhuru utahubiri namna gani, hata ufanye nini, haliwezi kuivishwa, haliwezi kudhihirishwa, haliwezi kuthibitishwa; ila tu na Yeye aliyesema, “Mimi Ndimi Nuru ya ulimwengu,” lile Neno. Kwa hiyo hakuna budi kutokee Nguvu fu—fu—fulani, Roho Mtakatifu Mwenyewe, kuivisha, ama

kuthibitisha, ama kuhakikisha, ama kudhihirisha ya kwamba yale ambayo Yeye amebashiri yangetukia katika siku hii. Nuru ya jioni inaleta hilo. Ni wakati wa jinsi gani!

⁵³ Bibi-arusi alipitia mahali pale pale alipopitia wakati alipokuwa hapo mwanzo. Lakini nilikuwa nikimwalia akitoka mstarini, na nikijaribu kumvuta arudi kwenye mstari. Sasa, mengi yangeweza kusemwa juu ya mambo haya, juu ya siku tunayoishi.

⁵⁴ Sasa, Hosea alisema, katika 6:1, “Mrudieni Bwana.” Kumbukeni, yeye alisema ya kwamba wangetawanyika, nao walitawanyika. Alisema, “Watamrudia Bwana, baada ya kutawanyika, Naye angeninii, atawafunga.” Angalia, “Rudini... Watatawanyika; la pili... Walikuwa wameraruliwa, na walipofushwa.” Hivyo ndivyo ilivyotukia hasa. “Yeye atatuponya, na atatufunga.”

Kama vile Ezekieli 37, “Ile mifupa mikavu, bonde lililojaa mifupa mikavu.” Ezekieli alikuona, kurudi kwao tena.

Halafu angalia, Hosea alisema, “Baada ya siku mbili! Baada ya siku mbili Yeye angewarudia. Atatupokea na kutupa, kutufufua.” Sasa, *kufufua* hakumaanishi “ufufuo.” *Kufufua*, hapo, ni neno lile lile linalotumika mahali pengine popote, ndiyo kwanza nilichunguze, linamaanisha, “uamsho.” “Yeye atatufufua baada ya siku mbili.” Hiyo ingekuwa, “Katika siku ya tatu Yeye atatufufua tena, baada ya kututawanya, na kutupofusha, na kuturarua.”

⁵⁵ Unajua, Wayahudi sana sana walipofushwa kusudi sisi tuweze kuona. Waliraruliwa, na kutawanywa, kama taifa, nao wakamkataa Masihi wao; tupate kumpokea Masihi huyo, kusudi kuwe na watu walioitwa kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake.

⁵⁶ Sasa, mwanamume anakuja, naye mwanamke anachukua jina lake. Hawa Mataifa waliopofushwa ambao hawawezi kuona Jina hilo, “Bwana Yesu Kristo,” katika ubatizo! Ni jambo baya sana, bali inabidi iwe hivyo. Wayahudi, iliwabidi kuninii—iliwabidi kutoona jambo hilo. Kuna mtu mmoja tu anayeweza kuona jambo hilo; huyo ni yule aliyekusudiwa tangu zamani kuliona. Vinginevyo hataliona kamwe.

Wayahudi hawangeweza kumwona huyo kwamba ni Masihi wao. Na, hata hivyo, walikuwa ni wanachuoni na wanathiolojia, watu mashuhuri sana katika masomo, waliosoma Biblia ii hii unayosoma wewe. Sasa, baada ya jambo hilo kutambulishwa kwetu, tunaweza kuliona dhahiri, huyo alikuwa ni Masihi. Lakini, wasingeweza kuona jambo hilo, wala hawawezi kuliona leo. Wametabiriwa kuwa vipofu, pia.

⁵⁷ Kanisa, siku hii, limetabiriwa kuwa kipofu, kuukataa Ujumbe wa wakati wa jioni. Ufunuo 3 ilisema hivyo, “Wewe ni mnyonge, mwenye mashaka,” angalia hali ya bibi-arusi hivi

majuzi usiku, ama kanisa, “uchi, kipofu, wala hujui.” Bwana Yesu, turehemu! Biblia ilisema lilikuwa “uchi.” Sijawahi kuliona hadi sasa hivi tu. Kanisa la Laodikia lilikuwa uchi. Na wakati lilipotokea hivi majuzi usiku, lilikuwa “uchi,” sijawahi kuliona hilo, “wala halikujua.”

⁵⁸ Loo, jinsi tunavyoshukuru! Jinsi, si ajabu tunashukuru sana! Ninajisikia kwamba hatuna shukrani vya kutosha kwa ajili ya mambo ambayo Mungu anatujulisha.

⁵⁹ “Uchi.” Na yale maono yalisema, yalinionyesha lilikuwa uchi wala halikujua, na “limepofushwa.” Kama vile Israeli walivyopofushwa ili kwamba Mataifa waweze kuingia, sasa Mataifa wamepofushwa ili Bibi-arusi aweze kutwaliwa na Israeli waweze kupokea sikukuu ya Baragumu. Kamilifu tu kabisa!

⁶⁰ “Baada ya siku mbili atatufufua, ama atatupa uamsho, akitukusanya pamoja, hao Wayahudi,” akinena kuhusu Baragumu hizi sasa. Naye ataninii. . . “Nasi tutaishi mbele ya uso Wake, ama tutakuwa na Uzima wa Milele. Unaona, tutakuwa mbele ya uso Wake.” Biblia ilisema hapa katika Hosea, ilisema, “Nasi tutaishi mbele Zake; Uzima, tutakuwa na Uzima mbele Zake.” Yaani Uhai Wake Mwenyewe, Uzima wa Milele, “tutapata Uzima mbele Zake.”

“Mwanamke asiyejizua nafsi yake amekufa ingawa yu hai.” Kwa hiyo sisi. . . aliahidi ya kwamba Israeli itapata Uzima tena mbele Zake. Walikuwa wamekufa, kwa zile kweli, na kwa sikukuu ya pentekoste.

⁶¹ Sasa angaliani, kwa makini. “Kisha baada ya siku mbili.” Sasa, hiyo haikumaanisha siku mbili zenye masaa ishirini na manne, kwa kuwa kulikuwa na. . . Hilo lilitukia huko nyuma kabisa, mamia kadhaa ya miaka iliyopita. Unaona? Lilimaanisha, “siku mbili kwa Bwana,” baada ya miaka elfu mbili. Sasa, mnajua imekuwa ni muda gani tangu wakati huo? Imekuwa ni miaka elfu mbili na mia saba tangu wakati huo, maana katika Hosea hapa ni mwaka wa 780 kabla ya Kristo. Mwaka wa 1964, unaona, imekuwa kitu kama zaidi ya miaka elfu mbili na mia saba iliyopita. Yeye alisema, “Baada ya siku mbili, katika siku ya tatu, Yeye atatuhuisha tena, na kutupa Uzima mbele Zake.” Hizo hapo Baragumu zenu zinaingia. Hiyo ndiyo saa tunayoishi, siku tunayoishi.

⁶² Sasa, wametawanyika, wamepofushwa, wamekusanyika, nao wameenda sana katika siku ya tatu. Unaona hilo? Walitawanyika, kutoka Palestina, kote ulimwenguni. Walipofushwa, wapate kumkataa Masihi. Na sasa wamekusanyika katika nchi ya uenyeji wao, wakiwa tayari kwa ajili ya zile Baragumu, wapate kuutambua ule Upatanisho.

Kama vile Biblia ilivyosema, “Wakati watakapoipokea, na kumwona akiwa na kovu za misumari,” baada ya Kanisa

kutwaliwa, “nao wanasema, ‘Ulipata wapi kovu hizi?’ Yeye alisema, ‘Katika nyumba ya rafiki Zangu.’” Naye akasema, “Watajitenga, kila jamaa, na watalia na kuomboleza, kwa siku nyingi, kama jamaa iliyopoteza mwana wao wa pekee.” Kumbukeni, hiyo sikukuu ya Baragumu ilikuwa ifanye hivyo. “Kulia, kuomboleza kwa ajili ya Dhabihu iliyochinjwa,” nao walikuwa wameikataa.

⁶³ Wako katika nchi yao. Walikuwa wametawanyika, wamepofushwa, na sasa wamekusanyika. Na yote yalikuwa chini ya Muhuri huo wa Sita, zile Baragumu zao Saba...zilipigwa zipate kuwakusanya pamoja, ile Baragaumu ya Sita. Ile ya Saba ni “ile Baragumu Kuu,” kama tulivyosema Jumapili iliyopita. Baragumu ya Sita ilipigwa chini ya Muhuri wa Sita. Kama vile tu Muhuri wetu wa Sita ulivyofunguliwa, kila kitu wakati ule ule; ila tu, zao zote zilipigwa mara moja; ambapo, sisi tumekuwa katika sikukuu ya pentekoste kwa miaka elfu mbili.

⁶⁴ Sasa, miaka elfu mbili mia saba tangu wakati huo. Alisema, “Katika siku ya tatu, tutakusanyika tena. Baada ya siku mbili, katika siku ya tatu, tutakusanyika tena, na kupokea Uzima mbele Zake.” Je! unaona hiyo ahadi? Majira yameandikwa kikamilifu ukutani. Tunaona mahali tunapoishi.

⁶⁵ Sasa katika nchi ya uenyeji, wakingojea Sikukuu ya Baragumu, ama kule kuutambua Upatanisho, na kungojea kule Kuja, kuomboleza kwa ajili ya ile mara ya kwanza walipoukataa. Wao wako kwenye nchi ya uenyeji wao kwa ajili ya jambo hilo, wakingojea. Wote wananinii...Kila kitu kimewekwa mahali pake.

⁶⁶ Kama mhudumu wa Injili, siwezi kuona jambo moja lililosalia ila kule kuondoka kwa Bibi-arusi. Na inapasa Bibi-arusi aondolewe kabla wao hawajaweza kutambua jambo ambalo limetukia. Walifungwa, wakatawanyika... Ninamaanisha, walitawanyika, wkapofushwa, na sasa wamekusanyika. Ni kitu gani kilichosalia? Bibi-arusi kuondolewa njiani. Wanangojlea kuondoka kwa Bibi-arusi, kusudi nabii wao wa Ufunuo 11 waweze kuwaita waje kwenye sikukuu ya Baragumu, kuwafanya watambue jambo ambalo wamefanya.

⁶⁷ Kumbukeni, papo hapo katikati ya hiyo Mihuri, kulitokea Muhuri wa Sita. Na kulikuwa na mia moja na arobaini na nne elfu, waliochaguliwa na kuitwa. Na kati ya Baragumu ya Sita na ya Saba, Ufunuo 11 inatokea papo hapo ikiambatana moja kwa moja na Muhuri wa Sita.

⁶⁸ Kufanya nini? Ulikuwa ufanye nini? Na hii ilikuwa iwaleta wale mashahidi wawili, Musa na Eliya, manabii. Ambapo, Wayahudi wanawaamini manabii wao peke yao. Nao watajitokeza wakiwa na ishara ya manabii, na kazi yao itakuwa ni ile ya nabii, kwa kuwa walifanya vivyo hivyo hasa.

Ikionyesha jambo moja, ya kwamba, mwanadamu, unapokufa ama chochote kile, unapoondoka humu ulimwenguni, tabia yako haibadiliki. Kama wewe ni mwongo sasa, utakuwa mwongo kule. Kama u mkali hapa, utakuwa mkali kule. Kama wewe ni mwenye kushuku hapa, utakuwa mwenye kushuku kule. Wanaume na wanawake, wakati umewadia wa kujitikisa na kujichunguza, na kuona mahali tunaposimama, kwa maana kifo hakibadilishi jambo hilo.

⁶⁹ Walikuwa wameondoka kwa miaka elfu mbili. Musa kwa muda wa miaka kama elfu mbili na mia tano, na Eliya tangu wakati huo. . . Eliya ameondoka kwa karibu muda wa miaka elfu mbili na mia tano, na Musa alikuwa hayupo, nao hawa hapa wanarudi wakiwa na tabia ile ile na kufanya mambo yale yale.

Kifo hakimfanyii mtu lolote ila tu ni kubadilisha makao yake. Hakibadilishi tabia yako. Hakibadilishi imani yako. Hakibadilishi kitu chochote ndani yako ila mahali unapoishi.

⁷⁰ Kwa hiyo, jinsi tabia yako ilivyo asubuhi ya leo! Kama wewe ni mwenye kushuku Neno la Mungu, utakuwa mwenye kushuku kule. Sijali wewe ni mtakatifu jinsi gani, jinsi unavyoishi, na jinsi unavyoishi vizuri, kifo hakingekubadilisha hata kidogo, ni mahali tu unapoishi. Na endapo huwezi kukubali Neno lote la Mungu jinsi lilivyoandikwa, hungelikubali Kule; kwa hiyo, usijali, hutakuwa Kule.

Huna budi kulikubali katika utimilifu Wake, katika nguvu za kuthibitishwa Kwake na ufunuo wa kile lilicho, ndipo unakuwa ni sehemu Yake. Yeye atafufua tu Neno Lake, kama alivyolifufua Neno Lake kwenye ile asubuhi ya Pasaka ya kwanza. Neno Lake ndilo tu lililofufuka, na wale waliokuwa wamekufa katika Neno Lake, wakiadini Neno Lake na kulithibitisha Neno Lake.

⁷¹ Angalia, sasa, hayo yamekuwa ni miaka elfu mbili na mia saba iliyopita. Angalia, wao walitawanyika, walipofushwa, na sasa wamekusanywa. Sasa, jambo linalofuata ni kwamba watapokea Uzima.

⁷² Na Mataifa wanaitwa watoke. Bibi-arusi yuko tayari. Kunyakuliwa kumekaribia. Je! tunaweza kutambua jambo hilo? Je! kweli tunaweza kuamini jambo hilo? Ni hadithi ambayo imesimuliwa? Ni hadithi ya uongo, kwetu sisi? Ni jambo ambalo linasikika kwamba ni la kweli? Ni jambo ambalo sisi, tulio nje, tunaweza kuamini? Ama, ni jambo ambalo limo ndani yetu, ambalo ni sehemu yetu, ambalo ni zaidi ya uhai kwetu? Je! tuko na msimamo wa aina gani, asubuhi ya leo, katika Maskani hii? Kumbukeni, litakalolipokea ni kundi dogo.

⁷³ Sasa katika nchi ya uenyeji, walingojea zile Baragumu. Sasa wanangojea kule kuondoka kwa Bibi-arusi mdogo, ili kwamba Ufunuo 11 ipate kutimizwa. Wakati wa kanisa umekoma; Mihuri imeisha kufunguliwa, ambayo inathibitisha yale waliyoacha

katika wakati wa kanisa, na Ujumbe umetolewa. Israeli iko uwanjani, haleluya, wakiwa tayari kwa ajili ya Sikukuu ya Baragumu.

⁷⁴ Loo, enyi watu mlio kwenye nchi nyingine ambako mtasikia kanda hii, hivi hamwezi kuamka, ndugu yangu? Ama, je! linakupofusha? Je! Ungeweza kulitupilia mbali na kuliita unabii wa uongo? Wakati, limethibitishwa moja kwa moja mbele zako, na ulimwengu, na wakati, na watu, na kwa Roho Mtakatifu ambaye aliliandika. Limethibitishwa, kwa njia za kawaida, za kiroho, kimwili. Kila kitu alichosema Yeye kimetimizwa na kuthibitishwa.

⁷⁵ Israeli nchini mwao; walisukumwa mle ndani, wakakusanywa waingie kule, kama kondoo. Mbwa mwitu waliwafukuza na kuwakimbiza wakarudi kwenye usalama, katika nchi yao wenyewe. Kumbukeni, Israeli imeahidiwa kubarikiwa mradi tu alikuwa kwenye nchi yake. Mungu kamwe hawabariki Israeli nje ya hiyo nchi. Ibrahimu alitoka nje ya nchi hiyo, akahukumiwa. Kila mtu anayeondoka humo nchini amelaaniwa. Mungu anaweza tu kuwabariki Israeli wakati wanapokaa katika nchi ya uenyeji wao, nao wako kule sasa kama taifa. Nalo Kanisa limeitwa; linangojea tu Kunyakuliwa, kwa Bibi-arusi kuondolewa.

⁷⁶ Ile Mihuri imefunguliwa. Imefunuliwa kwetu. Tunaona yale waliyoacha. Ninyi mnaotaka kujadiliana na kuzozana juu ya uzao wa nyoka, na ubatizo wa maji, na kadhalika, mmepofushwa wala hamjui. Mungu wa ulimwengu huu amewapofusha, kwa jambo Hilo, wala hamjui. Si ajabu nilikuwa na wakati mgumu sana asubuhi ya leo, nikipigana katika mashinikizo hayo!

⁷⁷ Kusudi manabii wao wapate kufunuliwa katika siku hii ya mwisho; haiwezekani, kwa Baragumu, za...kwa Sikukuu ya Baragumu.

⁷⁸ Yeye alisema, kupitia kwa Hosea, "Nimekata." Sasa angalia, anazungumza na Israeli. "Nimekata," ama kwa maneno mengine, "Nimewabangua, nimewabangua kabisa, kwa njia ya manabii." Hivyo ndivyo Mungu anavyowafanyia watu Wake. Aliwabangua akawatoa kutoka kwa mataifa mengine. Kwa kitu gani? Upanga Wake ukatao kuwili, Neno Lake. Yeye aliwabanja, taifa Lake, kutoka kwa mataifa. Alibangua taifa Lake kutoka kwa mataifa, kwa manabii, Neno Lake lililothibitishwa.

Vivyo hivyo Yeye amebangua Bibi-arusi Wake kutoka kwa madhehebu, kwa Neno Lake; lililoahidiwa na Malaki 4, katika siku ya mwisho. Akambangua akamtoa Bibi-arusi Wake, akamkatilia mbali na makanisa mengine! Alikata akamtoa Bibi-arusi Wake!

⁷⁹ Aliwakata, manabii Wake; kupitia, kwa manabii Wake, kwa Neno akawakata Israeli. "Jitengeni na hao wengine."

Angalia wakati walipotaka kutenda kama hao wengine. Walimjia nabii, Samweli. Yeye akasema, “Je! nimepata kuchukua fedha zenu? Je! nimewahi kusema nanyi katika jambo lolote, katika Jina la Bwana, ila lile lilitukia?”

Wao wakasema, “La, hiyo ni, hiyo ni kweli, bali tungali tunataka mfalme.”

⁸⁰ Hivyo ndivyo makanisa yamefanya. “Loo, tunaamini Neno. Ni sawa, bali, unajua, wao wanasema tunapaswa kufanya *hivi*.” Sijali wao wanasema nini. Neno ni sahihi!

Kungojea. Yeye amewakatilia mbali, kwa manabii.

⁸¹ Ni saa ngapi, ndugu? Ni saa ngapi, mhudumu? Je! unaona ni saa ngapi ya siku, na ishara unayoishi chini yake? Unaweza kufahamu jambo hilo? Unaliona?

⁸² Kila mahali sasa, hakuna ufufuo. Kila mtu analalamika, wahudumu wanalia. Nilikuwa nikisoma moja ya ma—magazeti maarufu sana yanayokuja hapa kanisani, gazeti zuri sana. Nami ninamjua mhariri wake, na ninawajua hao watu. Nao ni watu wacha Mungu, watu wazuri sana, Ndugu na Dada Moore, wa *Mbiu ya Kuja Kwake*. Moja ya magazeti yaliyo mazuri sana katika huduma, *Mbiu ya Kuja Kwake*. Lakini ni vigumu kwao kuchapisha jambo lolote isipokuwa lihusu, “Fungeni, ombeni! Fungeni, ombeni! Pigeni mbiu! Shikeni. . .” Ni wangapi wanaolisoma? Mnajua. Mnaliona wakati wote, “Fungeni, ombeni! Fungeni, ombeni!” Ndiyo tu unayosikia. “Fungeni, ombeni! Tutapata mapambazuko makubwa! Kuna jambo kubwa litakalotukia! Ninyi nyote, ombeni, ombeni, ombeni! Hatujachelewa sana bado.”

⁸³ Ni kwa nini wanafanya hivyo? Kwa nini wanafanya hivyo? Wanataka uamsho mkubwa. Wanalia, wakiadini ya kwamba kutakuwa na uamsho. Wao ni watu wazuri. Ni kwa nini? Wamefanya nini? Hawajatambua ule uamsho wa Bibi-arusi. Unaona? Kwa kuwa wao ni Wakristo, wanasikia ule mvuto wa saa hii, bali hawajatambua jambo ambalo limetendeka. Hilo ndilo linalowafanya wajisikie namna hiyo. Wanajua jambo fulani linapaswa kutukia, bali, unaona, wao wanalitazamia huko mbali kabisa katika siku zijazo, lipate kuja, wakati limetendeka moja kwa moja karibu na mahali ulipo wewe.

⁸⁴ Hilo ndilo jambo lile lile walilofanya katika siku za kale. Walikuwa wakiadini katika kuja kwa Masihi. Waliadini ya kwamba kungekuwa na mtangulizi atakayekuja. Lakini jambo hilo lilitukia moja kwa moja kwao, wala hawakujua. Hawakulitambua. Waliadini kungekuwa na mtangulizi atakayekuja ambaye angemtangulia Masihi, nao wakamkata kichwa. Kisha wakamwua Masihi wao, kwa maana ilikuwa imetabiriwa kwamba wangepofushwa. Hosea alisema jambo hilo.

⁸⁵ Na Roho yule yule, aliyenena kupitia kwa Hosea, alinena kupitia kwa Yohana na kusema kanisa katika siku hizi za mwisho lingekuwa “uchi, na kipofu, na lingemtoa nje ya kanisa.” Walishindwa kuona nabii hizo zikitimia. Lakini, wakiwa mle ndani, wanatambua ya kwamba jambo fulani halina budi kutendeka. Ni kwamba tu hawalipati. Hawalitambui. Ni kama vile wale Wayahudi wa nyakati za kale; Laodikia ilivyopofushwa; utajiri mwingi, thiolojia, inayochukia Kanisa, inayochukia Ujumbe huu. Angalia jinsi hao Wayahudi walivyomchukia Yohana. Angalia jinsi walivyomchukia Yesu, wakati alikuwa Ndiye hasa waliyedai kwamba walikuwa wanamtazamia.

[Mfumo wa kupaza sauti unatoa sauti ya kuvuma—Mh.] Ninaamini tumeunguza fyuzi. Nafikiri hiyo inakatiza vinasasauti, pia. Haikatizi. Vema.

⁸⁶ Walikuwa maadui wa Ujumbe.

Jambo ni kwamba, kuna nguvu nyingi sana; kila mmoja wenu ni mtambo unaotoa joto. Hakuna njia ya kuliweka kanisa katika hali ya kawaida kabisa katika hizo, chini ya nyakati hizo. Kwa maana, unaona, kila mmoja wenu ni BTU tisini na nane, kwa kawaida. Nanyi hamkai tu pale namna hiyo; daima mnatoa joto. Pana hewa ya kutosha hapa ndani sasa kupagandisha mahali hapa. Lakini, mtambo-joto ukiwa unafanya kazi, ha—hamwezi kufanya hivyo.

⁸⁷ Angalia adui! Lakini, sasa, kama vile wale Wayahudi wa kale, wamepofushwa! Wako kwenye Laodikia. Wao wako “uchi, wenye mashaka, wanyonge, wala hawajui.” Siku ya utajiri, mafundisho makuu ya kithiolojia, elimu kuu, na sasa wanauchukia Ujumbe. Hawataki uhusiano wowote Nao, kama tu ilivyokuwa huko nyuma katika siku ambazo Yesu wa Nazareti alipokuwa duniani.

⁸⁸ Sababu ya watu, katika siku za Nuhu, kutoingia katika safina, ni kwamba kamwe hawakuutambua ule ujumbe wala mjumbe wake. Hiyo ndiyo sababu pekee wao waliangamia, ni kwa sababu hawakutambua saa walivyokuwa wanaishi. Hawakutambua ya kwamba Mungu angeshughulikia dhambi kama alivyoahidi atafanya. “Atamwangamiza mwanadamu, kutoka katika uso wa nchi.” Yeye alikuwa ametabiri jambo hilo. Alilimaanisha. Naye analimaanisha hivi leo kama vile alivyolimaanisha wakati huo.

⁸⁹ Lakini watu, badala ya kumpenda Nuhu, yeye alihebiwa kwamba ni mwenda wazimu. Hawakuamini kwamba yeye ni nabii. Mnajua, Yesu, Yeye Mwenyewe, alitwambia jinsi walivyodhihaki katika siku za Nuhu, wakamdhihaki, wakamwita mshupavu wa dini na kadhalika. Bali hawakuutambua wakati wao. Hawakuitambua siku hiyo. Hawakuitambua ile ishara. Hawakuutambua ule ujumbe.

Hawakumtambua mjumbe, bali walimfukuza kati yao na kumcheka. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu!”

⁹⁰ Huku Israeli ikiwa katika nchi yake, na kila kitu kimekaa sawa sasa, na Ujumbe unaingia kikamilifu, je! tunaishi katika siku gani, ewe ndugu? Tuko wapi?

⁹¹ Hawakuijua ile siku. Hawakujua. Hiyo ndiyo sababu waliikosa, ni kwa sababu hawakuitambua. Walikuwa ni kama siku hizi, zaidi sana kama watu walivyo siku hizi, wamepofushwa na mathibitisho ya kisayansi, na mifumo ya elimu, na seminari za kithiolojia. Na mambo yaliyowapofusha katika siku hiyo, yamefanya jambo lile lile leo. Yamewapofusha, tena.

⁹² Na, pia, ule urahisi, urahisi wa ujumbe pamoja na mjumbe wake! Nuhu hakuwa wa kisayansi. Hakuwa mtu mwenye elimu. Alikuwa mkulima maskini, mnyenyekevu, akiwa na ujumbe rahisi. Ulikuwa ni rahisi sana kwa elimu yao ya juu.

Ndivyo ilivyo na leo hii! Mungu daima anaufanya rahisi, ili awapate watu watakaomwamini na kumtumaini. Ni tofauti, ni Ujumbe tofauti tu, bali ni Mungu yule yule. Sasa ninawatakeni muuamini Huo na mfahamu ya kwamba Mungu ameunena.

⁹³ Yesu alisema wao walimdhihaki nabii Wake, Nuhu. Nao kama walivyomdhihaki katika siku ile, ndivyo watakavyofanya tena kwenye kule Kuja Kwake. Wangefanya jambo lile lile.

Hiyo ndiyo sababu kwamba Farao alizama baharini. Yeye hakuitambua siku yake kamwe. Hakutambua yaliyokuwa yakiendelea. Alikuwa amechukuliwa mno na mafanikio ya wakati wake wa kisayansi, kujenga miji kwa kuwatumia watumwa. Alikuwa—alikuwa na shughuli nyingi sana, asingeweza kutambua nafasi aliyokuwa nayo, naye akamfukuza nabii-mjumbe wa Mungu aende zake nyikani. Hakuitambua. Hiyo ndiyo sababu kwamba mambo yalienda jinsi yalivyoenda. Yeye kamwe hakulitambua. Laiti angalitambua tu Neno la Mungu lililoahidiwa, kwa hao watu!

⁹⁴ Na kama makanisa leo yangetambua, kama makanisa yangetambua Neno la Mungu ambalo limetoa ahadi hii kwa ajili ya saa hii, kwa watu, wasingeamia.

Kama Marekani ingeweza kutambua katiba iliyoiandika, isingekubali kuondoa Biblia shuleni, kuondoa Jina la Mungu kwenye sarafu, na kuahidi kumtii Mungu. Lakini haiitambui. Kwa nini? Ni kipofu, uchi. Haiwezi ikatambua damu ya wale vijana wa thamani ambao wamefia vitani kwa ajili ya baraka hii. Wamesahauliwa; wao ni mavumbi.

⁹⁵ Bali kuna Mmoja ambaye anakumbuka damu iliyomwagika ya manabii, gharama iliyogharimu kuleta Injili hii kwetu leo. Jinsi ambavyo maelfu wameliwa na simba, na kutupwa

matunduni, wamekatwa kwa misumeno, wakachomwa moto, wakasulibiwa! Mungu anatambua jambo hilo.

Kanisa limesahau manabii wao. Wao “hawawahitaji tena,” ndivyo wanavyodai. Bali Mungu anajua hana budi kuwa nao; Yeye huwakata watu Wake kwa Neno Lake. Lakini kwao Hilo limepitwa na wakati sana katika siku hii. Hawalitambui. Hiyo ndiyo sababu wako katika hali waliyo nayo. Hiyo ndiyo sababu wao ni “uchi, wenye mashaka, vipofu, wanyonge, wala hawajui,” kwa kuwa hawaitambui saa tunayoishi. Hawaioni.

⁹⁶ Musa, yeye alitambua siku yake na wito wake, wakati alipoona ahadi ya Neno la Mungu kwa ajili ya siku hiyo ikithibitishwa. Yeye alijua basi, na kutambua kile alichokuwa na kile alichopaswa kufanya, kwa Neno lililoahidiwa. Kwa hiyo yeye hakuogopa yale mtu yeyote aliyosema. Hakuonea haya ujumbe wake, ingawaje kila kuhani na kila farao, kila kitu, kila utawala, haukukubaliana naye. Bali alitambua wakati alipoona hiyo Nuru, ile Nguzo ya Moto ikining’inia kwenye kile kijiti, na ikanena naye Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo, na kusema, “Nimekuita uende ukafanye jambo hilo.” Yeye hakuogopa ti—tishio kuu za mfalme. Alishuka akaenda kuwaleta hao watu kwenye kutoka, kama vile Neno la Mungu lilivyokuwa limeahidi.

⁹⁷ Alipoona ile ahadi imethibitishwa, aliwatayarisha watu kwa ajili ya kutoka kwao. Wakati gani? Wakati alipoona ahadi ya Mungu imethibitishwa. Kumbukeni, alikimbia na thiolojia yake; alikimbia pamoja na mafundisho yake. Bali hapo alipoona Neno la Mungu limedhihirishwa, alipoliona limethibitishwa, “MIMI NIKO AMBAYE NIKO,” ndipo hakujali yale ambayo mtu yeyote alisema. Hakuhofu kile ambacho Farao angeweza kumfanyia. Hakuhofu kile hao wengine wangepanya. Yeye alimcha Mungu tu, asije akamfahamu Mungu vibaya, ama kwa njia fulani huenda akamfahamu Mungu vibaya. Yeye hakuwaogopa watu na yale ambayo wangesema ama wangepanya. Alimcha Mungu tu, baada ya yeye kutambua ya kwamba lilikuwa ni Neno la Mungu.

⁹⁸ Asingeweza kufahamu jinsi ambavyo mtu kama Yeye angetumwa kule chini. Lakini wakati alipotambua, kwa Neno lililothibitishwa, kwamba ilikuwa ni kitu gani, basi hakuogopa amri za mfalme. Laiti ungaliweza tu kutambua, laiti sisi leo tungaliweza kutambua! Musa alitambua jambo hilo wakati alipoona Neno likithibitishwa, alipoona thibitisho limehakikishwa, yeye alikuwa tayari kwa ajili ya kutoka kwa watu.

Ayubu hakutambua kamwe kwamba ilikuwa ni Mungu. Mradi tu ibilisi anaweza—anaweza kukufanya wewe uamini wakati mwingine ya kwamba yale majaribio madogo unayopitia ni—ni Mungu lab-. . . akikuadhibu! Ilikuwa ni Mungu akijaribu kumwonyesha jambo fulani. Ayubu hakutambua jambo hilo

mpaka alipoona ono. Kama vile Musa; wakati Musa alipoona lile ono, ile Nguzo ya Moto kwenye kile kijiti, ilikuwa imethibitishwa. Na wakati . . .

Ayubu, katika swali lake, “Mtu akifa, anaweza kuishi tena? Ninaona mti ukifa, na unaishi tena. Ninaona ua likifa, na linaishi tena.” Hilo ndilo lililokuwa swali lake. “Bali mtu hulala, anaaga dunia, anaharibika. Wanawe wanakuja kumwombolezea, wala yeye hatambui. Loo, laiti ungalinificha kaburini mpaka hasira yako itakapopita!” Asingefahamu ni kwa nini ua lingekufa kisha likaishi tena, jinsi jani lingeaanguka kutoka mtini, lianguke chini, na kukaa ardhini, na kurudi tena katika majira ya kuchipua. Yeye alisema, “Mwanadamu huaga dunia, na anaenda wapi? Ninamwamini Mungu; lakini kunatokea nini kwa mwanadamu?”

⁹⁹ Lakini basi siku moja radi ikaanza kumulika, ngurumo zikaanza kunguruma, Roho akashuka juu ya nabii. Ndipo akaona kuja kwa Mtu Ambaye angeweza kuweka mkono Wake juu ya mtu mwenye dhambi, na Mungu mtakatifu, na kuiunganisha njia. Ndipo akapaza sauti, “Ninajua Mkombozi wangu yu hai! Ingawa mabuu ya ngozi yatauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu!” Yeye alitambua kwamba ufufuo ulikuwa ni nini.

¹⁰⁰ Balaamu hakumtambua yule Malaika mpaka nyumbu aliponena kwa lugha. Balaamu asingeweza kutambua ya kwamba Malaika alikuwa amesimama njiani mwake. Mhubiri kipofu asingeweza kutambua ya kwamba ilikuwa ni Mungu Ndiye aliyekuwa amesimama njiani, akijaribu kumzuia asiuze karama yake kwa fedha. Na wakati huyo nyumbu aliponena katika sauti ya binadamu, ndipo Balaamu akatambua ya kwamba ilikuwa ni Malaika amesimama njiani mwake, akijaribu kumzuia asifanye yale aliyokuwa akifanya.

¹⁰¹ Loo, enyi madhehebu mliopofushwa! Kama Mungu anaweza kumtumia nyumbu, ambaye ni bubu, kuzungumza katika lugha asiyojua, kumfunulia mhudumu ya kwamba ameacha njia, hivi hawezi kumtumia mtu kufanya jambo lile lile? Watu waliopufushwa!

¹⁰² Laiti Ahabu angalitambua siku yake, asingemhukumu yule nabii, Mikaya, akiwa na Neno la Mungu aliloahidiwa.

¹⁰³ Wakati Ahabu aliposimama pale siku ile, yeye na—na Yehoshafati. Na wakati walipokuwa na manabii mia nne huko nje wakitabiri, wakisema, “Kwea! Kila kitu ni sawa. Ahabu, unaishi katika dhambi. Ulituundia dhehebu kubwa! Sisi ni watu mashuhuri. Tuna huduma kuu. Sisi hapa, tuko makasisi mia nne waliofunzwa, ama manabii. Tuko mia nne, tuliofunzwa katika Neno na thiolojia. Tunajua mambo yote kuhusu jambo Hilo.”

¹⁰⁴ Kwa hiyo, sasa, ilithibitika wao hawakujua kila kitu juu ya jambo Hilo. Mtu yule waliyemwita mwenda wazimu, katika

kizazi kilichowatangulia. Eliya, nabii wa kweli wa Mungu, alikuwa ametabiri, “BWANA ASEMA HIVI, ‘Mbwa watairamba damu yako, Ahabu!’” Unaona?

¹⁰⁵ Lakini hao makuhani, manabii wa kujibunia, walifikiria walikuwa wamepanga mambo yote vizuri tu. Wakasema, “Baba Ibrahimu. . . ama, Baba Ahabu, kwea! Bwana yu pamoja nawe. Una Maandiko, kwa maana Mungu aliwapa Israeli nchi hii. Ni mali ya Israeli. Kwea! Bwana yu pamoja nawe.” Loo, jamani!

¹⁰⁶ Lakini, unajua, Yehoshafati, mtu ambaye hakuwa amechangamana na dhambi kama Ahabu alivyokuwa amefanya, aliona mambo tofauti kidogo. Akasema, “Je! hakuna mwingine?”

¹⁰⁷ Akasema, “Tuna mmoja hapa, ila ninamchukia.” Unaona? Mungu alikuwa akifanya nini? Akiwambangua watu wake watoke, kwa kumtumia nabii, tena. “Ninamchukia. Hafanyi kitu ila kunihukumu tu sikuzote. Nawe unajua mimi ni mtu mashuhuri. Nisingekuwa na seminari hii hapa chini kama nisingekuwa mwaminio mashuhuri. Nina watu waliofunzwa vizuri. Nimewaweka chini kule wakiwa na vitabu na Biblia, na kila kitu, kufundisha jambo hili. Nami ninajua wao ni watu mashuhuri.”

Lakini kama Ahabu angalikuwa ametambua kwamba jamaa huyo ni nani, maskini jamaa huyu aliyeonekana amevaa matambara mabovu, mwana wa Imla, aliyesimama pale, akimwambia, “BWANA ASEMA HIVI,” kamwe asingalifanya kosa hilo baya sana alilofanya. Bali alimhukumu Mikaya. Kamwe hakuninii. . .

Loo, enyi watu, tambueni wakati mnaoishi! Angalieni jambo ambalo limetukia. Angalieni yale yaliyoahidiwa. Tambueni siku mnaoishi.

¹⁰⁸ Laiti kanisa la kimadhehebu leo lingalitambua tu ni kwa nini linahukumiwa, na wafuasi wao wanawakimbia, kama vile Israeli kutoka Misri! Laiti madhehebu yangaliacha kulaumu kanda hizo, na wangezisikiliza! Nawe, mhubiri, unayesikiliza kanda hii, sikiliza! Kama ungalitambua saa unayoishi, kama ungalitambua ishara ya wakati huu, ungeona ni kwa nini watu wanayakimbia hayo madhehebu. Roho wa Bwana, anaita! “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu,” alisema Yesu, “asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alio nao Baba, katika nyakati zilizopita, alionipa Mimi, watakuja.”

¹⁰⁹ Ni kama maskini yule mwanamke kisimani, na yule kuhani, jinsi walivyokuwa tofauti! Maandishi ya mkono yako kwenye ukuta leo, tena. Wanayaona, bali hawayatambui.

¹¹⁰ Laiti Wayahudi wangelitambua ishara iliyoahidiwa ya Masihi wao, kulingana na nabii wao wa mwisho! Malaki 3 ilisema, “Tazama, ninatuma mjumbe Wangu mbele za

uso Wangu, naye ataitengeneza njia.” Nao walidai walikuwa wakimtarajia.

¹¹¹ I—inaenda sambamba jinsi gani hadi kufikia si—siku hii! Wanadai wanatazamia jambo fulani kutukia. Mekanisa yote yanaomba na kufunga, na kusema, “Sasa hebu na tuombe. Hebu na tukusanyike pamoja. Inatupasa kuwa na jambo fulani kubwa litakalotukia. Tunajua kuna jambo kubwa litakalotukia. Kanisa halina budi kujitayarisha.” Hilo ndilo wanaloombea.

¹¹² Hilo ndilo walilokuwa wakiombea kule. Ndipo akatokea Yohana Mbatizaji. Kwa sababu, yeye alikataa seminari zao, kwa maana alifanya kinyume na yale baba zao wamefundisha. Alitokea nyikani bila elimu. Alitokea bila ukosi wake kupinduliwa, kama vile ingesemwa leo. Alitokea bila lundo kubwa la thiolojia. Bali alikuja, akijua kwa ahadi ya Mungu ya kwamba alikuwa amtangaze Masihi.

Akasema, “Yeye amesimama katikati yenu sasa.” Nao walifikiri alikuwa kichaa, kwa kuwa hakutokea kwenye shule zao. Maandishi ya mkono yalikuwa kwenye ukuta, wala hawakujua. Walidai walikuwa wakikutazamia kuja kwa Mtu kama huyo; naye alikuwa papo hapo miongoni mwao. Nao hawakumtambua, ingawaje walisema walikuwa wakimtaazamia.

¹¹³ Na kama vile tu, kama vile Wayahudi, walivyo ndani yake, kama vile Mataifa na mambo yao, kwa kuwa jambo lile lile limetabiriwa, jambo lile lile. Walidai walikuwa wakimtarajia. Bali madhehebu sasa katika Mataifa, wakati wa Laodikia ni mpofu tu kama wao walivyokuwa, kwa sababu (nini?) imetabiriwa wangepofushwa. Halina budi kutimia.

¹¹⁴ Kama Israeli wangeweza tu kuitambua ishara yao, wangejua wakati wa kuonekana kwa Masihi ulikuwa umewadia. Laiti wangelitambua!

Mnajua, wa—wanafunzi walimwambia Yesu hivyo. “Kwa nini waandishi wanasema, ya kwamba, ‘inampasa Eliya kuja kwanza?’”

¹¹⁵ Ndipo Yesu akasema, “Eliya amekuja tayari, wala hawakumtambua. Ameisha kuja; nao tayari wamemuua. Walifanya sawasawa na vile hasa Maandiko yalivyosema wangepanya.”

¹¹⁶ Laiti wangelitambua, ya kwamba huyo “mwenda wazimu” aliyekemea maradufu kila kitu walichofanya, aliyekemea kila kitu walichokuwa wakifanya... Yeye alisema, “Enyi wanafiki! Msianze kuninii... Nyoka nyanini, enyi uzao wa nyoka, ni nani amewaonya kuikimbia hasira ijayo? Msianze kuwazia ndani yenu, ‘Tunaye Ibrahimu Baba yetu. Tuna *hiki, kile*, au *kinginecho*.’ Kwa maana nawaambia, Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.”

¹¹⁷ Msianze kuwazia ya kwamba mna Baraza la Ulimwengu mkononi mwenu, na mna wafuasi wake waliovalia nadhifu sana. Mungu aweza kutoka kwenye vichorochoro vya panya hapa kujiinulia watoto kulitimiza Neno Lake; malaya, wazurura mitaani, walevi, wacheza kamari. Yeye anaweza kufanya jambo hilo. Yeye angali ni Mungu.

¹¹⁸ Madhehebu yaliyopofushwa, kama vile Israeli waliopofushwa, wote wawili wametabiriwa kuwa hivyo. Mimi ninawaonyesha mifano sambamba, mpaka nitakapofikia mahali hapa ninapotaka sasa. Waliopofushwa, kama ma—madhehebu ya Mataifa ya Wakati ya Laodikia, walivyopofushwa siku hizi kama walivyopofushwa wakati huo.

¹¹⁹ Wakati wa Laodikia unapaswa kupokea Ujumbe! Malaki 4 ilisema wataupokea.

Lakini wao wanatafuta nini? “Madhehebu yetu yatauleta. Kama haupitii kwetu, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wa—Waassemblies, wa Umoja, kuna ninii...kama hatuuleti sisi, Huo si wa kweli.”

Walifanya jambo lile lile siku ile! Nao ukaja na ukapita, wala hawakujua. Hawakuutambua, ingawa ulitimiza kila Neno. Yesu alisema, “Walifanya kama ilivyoandikwa kwamba watafanya. Ndivyo watakavyomfanyia Mwana wa Adamu,” atakataliwa.

¹²⁰ Sasa angalia, ni jambo lile lile sasa katika siku za Mataifa, kulingana na Maandiko yaliyoahidiwa ya Malaki 4.

Ambalo, Yesu alisema, “Maandiko yote yamevuviwa, wala hakuna hata sehemu Yake moja isiyoweza kutimia.” Hakuna njia ya kuyazuia Maandiko yasitimie. Yote hayana budi kutimia. Na Yesu alisema yatatimia. Na hapa tunaona likitukia. Tunaona jambo hilo.

¹²¹ “Kurejesha” nini, katika siku hii ya mwisho? Ninyi ndugu wa kimadhehebu, sikilizeni! Kurejeshwa kwa karamu ya kipentekoste, ya asili. Kama ilivyokuwa pale mwanzo, ndivyo itakavyorejeshwa kabla ya kupigwa kwa Baragumu ya sikukuu ya Israeli. Haina budi kurejeshwa! Kunapaswa kuwe na kitu cha kufanya jambo hilo. Malaki 4 ilisema ingerejesha Imani ya baba, iwaelekee watoto, yale ambayo yangetukia.

¹²² Kama Israeli wangelimtambua Masihi wao, ishara iliyoahidiwa, wasingekuwa mahali walipo siku hizi. Kama wangeninii... Lakini kwa nini hawakufanya hivyo? Ni jambo la kuhuzunisha. Kwa nini hawakumtambua? Kwa sababu Mungu alisema hawatamtambua. Ni wangapi wanaamini jambo hilo, semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Mungu alisema hawatamtambua.

Na ni Mungu yule yule aliyesema, katika Wakati wa Kanisa la Laodikia, jambo hili lingetukia, nalo hili hapa mbele zao. Wanawezaje kufanya jambo lolote ila kulitimiza.

¹²³ Laiti wangelitambua ishara iliyoahidiwa ya Masihi, ile ishara ya Mwana wa Adamu! Yeye alikuja katika Jina la Mwana wa Adamu. Sasa, Yeye alikuwa katika jina, katika Wakati wa Kipentekoste, katika Roho Mtakatifu, Mwana wa Mungu. Sasa, kitu kinachofuata ni ule Utawala wa Miaka Elfu, Mwana wa Daudi. “Wana” watatu, Mungu yule yule. Yule yule, “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” Mungu yule yule. Mwana wa Daudi, Mwana wa Mungu. . . Mwana wa Daudi, Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, ni Mungu yule yule wakati wote, katika huduma tatu mbalimbali tu za madaraka.

¹²⁴ Vivyo hivyo “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” si Miungu watatu, bali ni Mungu yule yule katika vipindi vitatu mbalimbali vya wakati, huduma tatu za madaraka, kama vile Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

Lakini, kama ilivyo siku hizi, wamepofushwa na mapokeo kama walivyokuwa wakati ule, wamepofushwa kimapokeo, hawalioni. Kwa nini wasiweze kuliona? Kamwe hawataliona. Kumbukeni, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

Mnasema, “Kwa nini unasema jambo hilo basi?”

Kama tu vile Yohana alivyofanya, kama na vile vile wengine wao walivyofanya. Kuna mmoja anayetokeza hapa na pale, ambaye hana budi kutolewa. Loo, enyi kondoo za Mungu, sikilizeni Sauti ya Mungu! “Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu.”

¹²⁵ Yule mwanamke kisimani aliitambua siku yake, kwa ishara ya Masihi. Yeye alikuwa katika hali mbaya. Hakutaka kujipumbaza na hayo makanisa ya kale, jinsi walivyokuwa wakitenda. Walikuwa wakiishi kwa kila njia, na, mambo waliyokuwa wakifanya, yeye hakuamini upuuzi huo. Lakini yeye alijua siku moja Mtu fulani angekuja. Maskini jamaa huyo kule juu, akielekea kisimani; yeye alipata kile Kitu alichokuwa akitafuta, wakati Yeye alipoanza kumfunulia siri ya moyo wake, akamwambia ile dhambi aliyokuwa akiishi nayo.

Akasema, “Bwana, mimi ninatambua ya kwamba Wewe ni Nabii.” Sasa, hawakuwa na nabii kwa muda wa miaka mia nne. Kasema, “Ninatambua ya kwamba Wewe ni Nabii. Nami ninajua ya kuwa Masihi ajapo Yeye atafanya mambo haya.”

Yeye akasema, “Mimi Ndiye.”

¹²⁶ Alitambua. Hakukuwa na swali lingine, “Unawezaje kuthibitisha jambo hilo?” Lilikuwa limethibitishwa tayari. “Masihi ajapo, hivi ndivyo atakavyofanya.”

Vema, kama yeye anaweza kutambua jambo hilo kwa Maandiko, je! hatuwezi kutambua Nuru za jioni na ishara ya leo hii?

“Tunajua Masihi ajapo Yeye atatuonyesha haya mambo yote. Atatwambia jambo hili.”

Yeye akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹²⁷ Hakuna swali zadi. Huyoo akaenda zake, naye akawaambia watu, “Njoni, mwone! Huyu hapa!” Hakuna swali lingine kwake. Lilikuwa limetatuliwa, kwa sababu yeye alitambua siku aliyokuwa anaishi. Aliitambua.

¹²⁸ Vivyo hivyo Nathanaeli pia, Mwebrania mashuhuri, wakati alipoona hiyo ishara ya Masihi iliyoahidiwa pale; haidhuru ni makuhani wangapi, ni wangapi chochote kile.

Ilifanyaje? Iliwasumbua makuhani, kuona hao watu wakiondoka makanisani na kwenda zao. Akasema, “Kama yeyote wenu akihudhuria mikutano Yake, mtatengwa na ushirika. Tutawafukuza moja kwa moja kutoka katika dhehebu.”

¹²⁹ Ndivyo ilivyo leo. “Tutakufukuza katika shirika letu kama ukihudhuria mkutano wake.”

¹³⁰ Mnakumbuka yule kipofu? Hata Baba na mama wasingeweza kujibu; walihofu. Kwa sababu, wao walisema, “Mtu yeyote aliyeenda kumwona Yesu, ama—ama kuhudhuria mikutano Yake, wangetengwa na ushirika.” Lakini, yule kipofu angeweza kujitetea, yeye aliyekuwa kipofu wakati mmoja angeweza kuona basi.

¹³¹ Mimi, ambaye wakati mmoja nilikuwa kipofu, sasa ninaweza kuona. Mimi, ambaye sikujua mambo haya, nimejulishwa haya na Roho Mtakatifu. Wafungulieni, enyi madhehebu, kwa sababu wao wanakuja, hata hivyo! “Nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta watu wote Kwangu.”

¹³² Nathanaeli alitambua jambo hilo. Alilijua.

¹³³ Ni kama tu mathibitisho ya Kimaandiko ya Musa, Neno lililothibitishwa. Musa alijua ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ahadi ya siku hiyo, kwa maana ilikuwa ni ya Kimaandiko, haidhuru ni jambo geni vipi. Akasema, “Niwaambie ni nani. . . Nitawaambia niliona Nuru huku nyuma nyikani. Ninawezaje kuwaambia sasa ya kwamba kulikuwa na Nuru huku nyuma, na Nuru hii ikaniambia nishuke niende kule?”

Akasema, “Hakika, Musa, nitakuwa pamoja nawe.” Na si ninii tu. . .

¹³⁴ Yeye hakujidhihirisha huko Misri; ila tu kwa miujiza tu na ishara. Bali alipowakusanya wote pamoja, aliwatokea tena, na kuthibitisha huduma ya Musa mbele ya Wateule na walioitwa watoke. Wakati nabii huyo alipokuwa amewakata kutoka katika taifa hilo na kuwaleta mahali fulani, ndipo ile Nguzo ya Moto ikatokea tena, pia na juu ya Mlima Sinai.

¹³⁵ Linganisha hilo na siku hizi. Hmm. Amina! Mungu asifiwe! Ni zaidi ya uhai kwangu. Na umri wangu unapoanza kunyemelea, na ninaona saa ya ushenzi huu na ufiisadi ikisambaa nchini na kadhalika, ndipo ninaangalia nyuma na kuona

jambo lililotukia. Moyo wangu unaruka kwa furaha, nikijua ya kwamba baada ya kitambo kidogo maskani hii iliyo ya makazi ya duniani itaharibiwa, bali nina moja inayongoja huko ng'ambo. Ninajaribu kuwavuta watu fulani, kuwakata niwaondoe kwenye mambo haya na kadhalika, kuwavuta watoke; kuwaonyesha, kwa Maandiko, ya kwamba Mungu amesimama pale; pamoja na thibitisho la Nguzo ya Moto, ambayo mamia na maelfu wameiona, na hata ilipigwa picha, hapo awali, kwa kamera, wakati baada ya wakati, kuthibitisha jambo hilo.

¹³⁶ Waigaji wanainuka. Hakika, halina budi kutukia. Waigaji waliinuka katika siku za Musa na kufanya jambo lile lile. Mungu alisema, "Jitenge, Musa. Usikae karibu nao. Nitawameza." Ndipo ulimwengu ukawachukua. Na ndivyo ilivyo siku hizi; wanarudi moja kwa moja ulimwenguni, miradi ya fedha na chochote kile. Unaona?

¹³⁷ Ishara ya Kiamaandiko ya Musa! Yeye alikuwa—yeye alikuwa ndiye yule nabii mkuu wa Mungu aliyeshuka akaenda kule kuwakomboa, nao wakatambua jambo hilo. Wakatambua ile ishara. Yeye alikuwa ni ahadi halisi ya Maandiko, iliyothibitishwa.

¹³⁸ Yesu alikuwa ndiye ile ahadi ya Maandiko, iliyothibitishwa kwa yule mwanamke. Ama, Yeye alikuwa ndiye hiyo Tafsiri. Yesu alikuwa ni Tafsiri ya Maandiko. Maisha Yake Mwenyewe yalifasiri Maandiko.

¹³⁹ Hivi hamwoni Ujumbe wa wakati huu? Je! mnaweza kutambua mahali tulipo? Ujumbe wenyewe, kutoka katika Maandiko, unawafasiria ile saa tunayoishi. Ndiyo tafsiri yake.

¹⁴⁰ Yesu aliwaambia Israeli, "Laiti tu mngalijua siku yenu." Wakati mmoja, alipokuwa ameketi juu ya Mlima wa Mizeituni, aliangalia huko, akasema, "Yerusalemu, Ee Yerusalemu!" Akalia. Akaangalia huko chini. Akaona.

Si kwa ulinganisho wowote, labda, njia ya kuliendea. Hivi majuzi usiku, hivi majuzi asubuhi, yapata saa nne, nilipoliona lile kanisa kahaba. Ndani ya moyo wako, unamsikia Roho Mtakatifu akitoa machozi.

"Yerusalemu, Ee Yerusalemu, ni mara ngapi ningekufunika. Bali ulifanya nini? Uliwaua manabii niliokutumia. Ukawaua kinyama."

Na Jumbe zilizotumwa kanisani, leo, zimeuawa na mafundisho yao ya sharti ya kimadhehebu. Maandiko yameuawa na mafundisho yao ya sharti. Yesu alisema, "Laiti mngalijua siku yenu! Bali, muda umeenda sana sasa, imeenda sana sasa." Ndivyo ilivyo kwa makanisa!

¹⁴¹ Ninaamini, kwa moyo wangu wote, limevuka mpaka wa ukombozi. Haidhuru unataka kuwazia jambo gani juu yake, hayo ni maoni yako. *Haya* ni yangu. Unaona? Si lazima

uchukue maoni yangu. Lakini ninaamini limevuka mpaka wa ukombozi, na limekuwa hivyo, kwa miaka mitano ama sita iliyopita. Ninakumbuka. Mnakumbuka huko Chicago. Angalieni yaliyotukia tangu wakati huo, na mwangalie yakiendelea kutukia. Unaona? Kumbukeni, jina langu liko mbele yake. Limebandikwa kule. Ni BWANA ASEMA HIVI. Angalieni kama halijaanguka, kuendelea kuanguka.

¹⁴² Angalia katika mwaka wa 1933, jinsi lilivyosema wanawake wangetenda katika siku hizi za mwisho. Jinsi lilivyosema watu. . . Jinsi ambavyo Mussolini, jinsi angefikia mwisho wake. Jinsi ambavyo Hitler angefikia mwisho usiojulikana. Jinsi ambavyo zile itikadi tatu zingeishia katika ukomunisti. Jinsi ambavyo mashine zingekuja, zikifanana na yai. Na jinsi ambayo wanawake wangevaa mavazi na kufanana na mwanamume, hata na kama vile nguo zao za ndani; na hatimaye wangevaa majani ya mtini, vitu kama hivyo, wajivike. Jinsi ambavyo tendo la uzinzi, jinsi ambavyo wangetenda leo hii. Angalia vile wamefanya. Na jambo hilo liko moja kwa moja mbele zenu, basi.

¹⁴³ Laiti wanawake Wakristo wangaliweza kuninii tu. . . hao wanaojiita wanawake Wakristo wangepewa kutambua tu, laiti wangepewa kutambua hiyo roho ya uzinzi iliyoko juu yao ni ya ibilisi, ya kuwafanya wakate nywele zao. Ibilisi ndiye pekee anayeweza kufanya jambo hilo. Hilo ni kinyume cha Neno la Mungu kwenu, kama tu ilivyokuwa katika bustani ya Edeni. Walifanya nini? Laiti tu wangaliweza kutambua! Wao wanajaribu kusema, "Loo, maskini mhubiri huyo mtakatifu anayejifingirisha, anasema!" Si mimi. Siwaambii la kufanya. Mimi ninanukuu tu Neno. Laiti wangaliweza kutambua ya kwamba ni ibilisi.

¹⁴⁴ Wanajiita Wakristo. Yesu alisema, "Mnawezaje kuniita Mimi, 'Bwana,' wala hamfanyi yale nisemayo mfanye?" Hawawezi kuwa Wakristo. Mimi si hakimu wao, bali ninasema tu vile Neno lilivyosema. "Mnawezaje kuniita, 'Bwana,' na halafu msifanye mambo niliyosema mfanye?" Na Neno lote zima hapa ni Ufunuo wa Yesu Kristo. "Mnaniitaje, 'Bwana'?"

¹⁴⁵ Laiti wangepewa kutambua kwamba ni ibilisi, roho ya uzinzi. Maskini wanawake wazuri huko nje. . .

¹⁴⁶ Nafikiri hapa ndipo mahali pashenzi sana nilipopata kuona maishani mwangu, Jeffersonville, Indiana, kwa wanawake walio uchi. Nimekuwa Hollywood. Nimefika kila mahali. Nimekuwa kote duniani, na nimeona kila namna ya uchafu. Nimeuona huko Paris. Nimeuona huko Uingereza, ambayo ndiyo kiongozi wao hao wote.

¹⁴⁷ Ninafikiri Uingereza itazamishwa siku moja chini ya bahari. Inastahili jambo hilo; uchafu, kinyaa, ufisadi! Hiyo ni shimo la maovu ya uzinzi wa ulimwengu, watu wanaoyapinga na

kuyakana Maandiko sana kuliko wote niliopata kuona maishani mwangu. Imekuwa hivyo kwa sababu imekataa ile Kweli.

¹⁴⁸ Billy Graham alisema ilimbidi kumwondoa mke wake kutoka kwenye zile bustani; mambo ya uzinzi yakitendeka kati ya wanaume na wanawake, wavulana kwa wasichana, papo hapo kwenye hizo bustani, waziwazi. Imekuwa shimo la uchafu; vivyo hivyo na Ufaransa pia, vivyo hivyo na ulimwengu uliosalia. Vivyo hivyo na Marekani, inakuwa kiongozi wa hizo nyingine zote!

¹⁴⁹ Angalia leo. Kuwafanya wakate nywele zao, wavae kaptura, suruali zinazopwaya, wavute sigara, na kujiita waaminio. Hivi hutambui, ewe dada, ama mwanamke... Namaanisha, samahani, si dada yangu; kufanya jambo kama hilo. Hivi hutambui ni ibilisi? Lakini nini. . .

Kama vile Wayahudi wa kale, hamtaamini Neno lililothibitishwa wakati limethibitishwa kwenu. Mnashikilia moja kwa moja kwenye mapokeo yenu ya kimadhehebu yanayosema kwamba ni sawa. Mnanena kwa lugha, mnarukaruka, mnaimba katika roho, na kukata nywele zenu. Je! mngeweza kuwaza Mkristo akifanya jambo hilo?

Nimeona pepo, nimeona wachawi, nimewaona wakinena kwa lugha na kufasiri, na kurukaruka na kucheza katika roho; wanakunywa damu kutoka katika fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kulaani Jina la Yesu Kristo.

¹⁵⁰ Unasema, “Mimi ni mfuasi wa kanisa. Haleluya! Utukufu kwa Mungu! Mimi. . .” Ati wewe ni mfuasi wa nini?

Kanisa ni Neno! Nalo Neno linasema, “Ni aibu kwako kufanya jambo hilo.”

Enyi kundi la Mafarisayo mliopofushwa, mnaowaongoza maskini watoto hao kwenda jehanamu namna hiyo; kwa sababu mnahofia posho, na kwamba mngufukuzwa kwenye madhehebu yenu kama mkianzisha kitu fulani kuhusu jambo Hilo. Aibu kwako, ewe mnafiki! Unalionea aibu. Unapoona ile saa ikikaribia namna hii, nawe kwa mapokeo yenu unaliacha Neno la Mungu. Unathubutuje, ewe kipofu!

¹⁵¹ Je! Biblia haisemi mlipofushwa? Hivi hamwezi kufahamu ya kwamba ninyi ni vipofu? Biblia ilisema mlikuwa vipofu. “Na wewe uko uchi, mwenye mashaka, mnyonge, kipofu, wala hujui.” Unapofikiri ya kwamba una kanisa lililo kubwa kuliko yote mjini, na unafanya *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*; na Biblia ilisema wewe ni maskini uwezavyo kuwa, na ni kipofu. Naye angali anasimama mlangoni, akijaribu kukuuzia dawa ya macho; si kukuuzia, bali kukupa, wala hutaki kuipokea. Unatimiza Maandiko.

¹⁵² Mnaishi katika siku gani, enyi watu? Je! mnatambua hiyo saa, mnatambua hiyo ishara?

¹⁵³ Laiti tu wangelitambua, hao wanawake, ya kwamba huyo ni ibilisi. Ni pepo mchafu, katika jina la dini. Amekuwa hivyo daima. Yeye alimjia kila nabii, alimjia kila mwenye hekima, hata alimjia Yesu Kristo, kama mtu wa dini. Na Biblia ilisema “angefanana sana katika siku za mwisho,” hata Wapentekoste, “na angewadanganya walio wateule,” kutoka katika hilo kanisa la Kipentekoste, “kama yamkini.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁵⁴ “Wachache,” Yeye alisema, “maana mlango ni mwembamba na njia imesonga, na bali ni wachache watakaonia. Kwa kuwa kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa, ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana wa Adamu.” Wazia jambo hilo! Tunaishi katika siku gani? Je! unatambua hiyo saa, unatambua hiyo siku?

Ninachukua wakati wenu mwingi sana, lakini nina dakika zingine chache. Unaona?

¹⁵⁵ Akiwafanya wakate nywele zao. Vema, wao wanasema, “Kanisa letu halijali jambo hilo.” Mnajua ni kwa nini? Wao ni vipofu.

“Hakuna madhara kwa kukata nywele zako.” Biblia inasema yapo! Hata ni kukosa adabu kwako kukata nywele zako kisha hata na uombe.

Unasema, “Vema, mwanamke anapaswa kufunikwa.” Na Biblia ilisema ya kwamba “nywele” zake ndizo kifuniko chake. Si kofia; nywele zake!

¹⁵⁶ Vipi kama Musa angalisema, “Nitavua kofia yangu badala ya viatu vyangu”? Isingekubalika. Mungu alisema “viatu,” na Mungu alimaanisha viatu.

Yeye alisema “nywele,” si kofia! Utukufu kwa Mungu! Yeye alipenda hilo, nina hakika. Mungu na apewe sifa! Yeye humaanisha vile anavyosema hasa. Maandiko si ya kufasiriwa apendavyo mtu binafsi. Haimaanishi kwamba ni kwa ajili ya madhehebu yako pekee; linamaanisha vile tu linavyosema, Naye ndiye mfasiri.

¹⁵⁷ Unasema, “Ninajua mwanamke anayefanya jambo hilo.” Sijali unalojua. Ninajua vile Mungu alivyosema juu ya jambo hilo. Fanya upendavyo.

¹⁵⁸ Laiti tu wangeweza kutambua ni kitu gani, ewe bibi. Loo! Laiti ungeweza kutambua! Ama, “mwanamke,” si bibi.

¹⁵⁹ Niliona ishara, nilipokuwa nikishuka kuja kutoka kwenye Blue Boar, kule chini, ninaamini ni kwenye Barabara ya Tano kule, kwenye baa fulani ya pombe, iliyosema, “Meza za mabibi.” Nilisimama tu pale; nikasema, “Hamjapata kuwa na mmoja.” Bibi hataenda mahali kama hapo. Huenda mwanamke akaenda, bali sio bibi.

160 Je! ulitambua, kuanguka kwa ulimwengu kulianzia na uzinzi wa mwanamke? Unajua utaishia kwa jinsi hiyo hiyo, uzinzi wa mwanamke? Na kanisa, linawakilishwa, na mwanamke? Kanisa ni mwanamke, tukizungumza kiroho.

Vivyo hivyo Bibi-arusi ni mwanamke, tukinena kiroho.

161 Uzinzi wa kanisa, jinsi limefanya! Angalia hayo maono, angalia hayo mambo, angalia hata maono ambayo Mungu anatoa, na ono hilo ni kweli. Nimeweka Biblia yangu moyoni mwangu, kwenu ninyi watu kwenye kanda, na wasikilizaji wanaweza kuiona. Niliona jambo hilo! Mwenyezi Mungu anajua hiyo ni Kweli. Sijapata kujua jambo hilo mpaka hivi sasa tu. Hilo hapo, “kipofu, wala halijui.” Lilikuwa tu likijifurahisha. Haya basi.

Bali wakati maskini Bibi-arusi huyo alipotokea, ilikuwa ni tofauti. “Yule Alfa na Omega!” A-ha.

162 Ibilisi hufanya jambo hilo. Lakini kama wale Wayahudi wa kale, wakiisha kuliona Neno . . .

Ndipo Yesu akawaambia ninii Wake, aliwaambia wanafunzi Wake hivi, “Yachunguzeni Maandiko. Ninyi, ninyi mnajua, mnashangaa juu Yangu Mimi na huduma Yangu. Yachunguzeni Maandiko. Ndani yake mnadhani mna Uzima wa Milele, nayo yananishuhudia Mimi, yanawaambia Ujumbe Wangu ni nini. Kama hamwezi kuniadini Mimi, aminini Maneno yenyewe ambayo Mungu anawafasiria.”

163 “Hatutaki Mtu huyu atutawale. Tuna makuhani wetu wenyewe, na kadhalika.” Endeeleni basi, hayo tu ndiyo yanayoweza kusemwa. Muda umeisha kupita, hata hivyo. Unaona? Mapokeo ya kimadhehebu yanayosema ni sawa, wao wanasikiliza hayo. Afadhali wasikilize. . . Mnaamini ne—neni la—la mwanadamu zaidi kuliko mnavyoamini Neno la Mungu. Hawatambui. Makanisa siku hizi hayatambui Timotheo wa Pili 3. Kama uki- . . .

164 Ninaona baadhi yenu mkiyaandika Maandiko hayo. Sasa, haya ni Maandiko ninayonukuu kutoka papa hapa. Ambapo, kama mtu yeyote akinirejesha kwake, ama kunipa changamoto kuyahusu, ninaweza kuwaonyesha Maandiko yake. Unaona?

165 Hawatambui Timotheo wa Pili 3, ambapo ilisema, “Katika siku za mwisho, watu watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizua, na wasiowapenda walio wema (Bibi-arusi), unaona; wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake; hao nao ujepushe nao. Kwa maana hao ndio wale watakaopita nyumba hadi nyumba, na kuwachukua wanawake wajinga, wanawake wajinga waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi, hawajifunzi kabisa ama hawawezi kuufikia ujuzi wa Kweli.” Kamwe! Wasingeweza kufanya jambo hilo, wala hawatalifanya. Mungu alisema hivyo.

Na, ewe Farisayo kipofu, hivi huwezi kuona jambo hilo? Mimi sijakasirika; ninapigilia tu msumari na kuukaza. Wala makanisa hayautambui Huu. Wanawake hawawezi kuufahamu. Wanapaswa... “Wanawake wajinga, waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi.” Hollywood, upuuzi wa namna hii yote, nywele zilizokatwa, wakivaa kaptura, wakijipodoa, upuuzi wote wa aina hii, ambao haufai. Je! mnajua mwanamke anashiriki sehemu kubwa katika siku za mwisho?

¹⁶⁶ Je! unajua Biblia ilisema, ya kwamba, “Hao watakaoepuka laana hii kubwa watakuwa tawi zuri mbele za Bwana”? Siku moja nitalifikia, Bwana akipenda, kwa ajili yake, kwa ajili yenu wanawake. Niwaache mwone vile Mungu anavyofikiri juu ya mwanamke ambaye kweli ataepuka laana hii ya siku hii. Kasema, “Atakuwa wa kupendeza.”

¹⁶⁷ Nilimsikia mwanamke, hivi majuzi, akicheka ninii... Msichana, kundi la wanawake nusu uchi, wenye uadilifu mdogo kuliko—kuliko mama mbwa, wakimcheka mwanamke mzee mwenye nguo ndefu. Sikiliza hapa, ewe msichana uliyepotoka, huyo ana kitu fulani usichojua lolote kukihusu. Ana uadilifu. Wewe hata hujui hilo jina lina maana gani. Uliupoteza kwenye tenga, utotoni, karibu utotoni. Hata hujui mema na mabaya; yeye anajua. Ana kitu fulani kilichofichwa moyoni mwake ambacho hujui lolote kukihusu. Uliupoteza; huwezi kuupata kamwe. Usimwite wa mtindo wa kale, na kadhalika, namna hiyo. Yeye anajua kitu fulani usichojua lolote juu yake. Yeye ameficha moyoni mwake, hazina ya uadilifu. Wewe hujui hata neno moja juu yake. Mama yako alikulea namna hiyo. Mchungaji wako aliruhusu jambo hilo; inaonyesha mahali anaposimama. Ninahubiri juu yake papa hapa sasa. Unaona? Unaona mahali mlipo, makanisa?

¹⁶⁸ Yesu alisema, “Maandiko yote haya hayana budi kutimizwa.” Na yametimizwa.

¹⁶⁹ Angalia, “Kama vile Yane na Yambre pia walivyompinga Musa,” yeye atakuja moja kwa moja, baadhi yao. Si, sasa, yeye hazungumzi kuhusu Mmethodisti, Mbaptisti, hapa; wao wako nje ya picha. Unaona? “Lakini kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa na Haruni, vivyo hivyo hao nao; watu walioharibikiwa na akili zao kuhusu ile Kweli.” wamepotoka wakaingia katika mafundisho ya sharti na mafundisho ya kanisa, badala ya Biblia.

Na halafu Yane na Yambre wangeweza kufanya jambo lolote ambalo Musa angefanya. Unaona, “kama vile Yambre,” unaona ulinganifu hapo?

“Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, vivyo hivyo na watu hawa walioharibikiwa akili zao kuhusu ile Kweli, wanavyokataa,” hawautaki karibu na maeneo wanayokaa, hata hawatashirikiana Nao, hawatataka uhusiano

wowote nao. Lakini akasema, “Upumbavu wao utajulikana.” Wakati Bibi-arusi huyo atakapochukua msimamo Wake na kwenda mbinguni, itajulikana, msijali; kama vile Musa, wakati alipowachukua wana wa Israeli, na kuhama Misri upesi, ndipo Misri ikazama. Vema.

¹⁷⁰ Yesu alisema, “Maandiko yote yana pumzi, kwa hiyo ni kwamba Maandiko yote hayana budi kutimizwa.” Wakati Yeye...

Wao walimwuliza, wakasema, “Unajifanya Mungu.”

¹⁷¹ Yeye akasema, “Ninyi, katika torati yenu, mnawaita hao manabii ambao walijiliwa na Neno la Bwana, mliwaita ‘miungu,’ nao ndivyo walivyo.” Kasema, “Basi mnaweza kunihukumu ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?” Maandiko yote haya yana pumzi; yote hayana budi kudhihirishwa, yote hayana budi kutimizwa.”

Unaona hapo, wao ni vipofu sana, walikuwa wakishughulika sana na neno la mwanadamu badala ya kushughulikia Neno la Mungu. Hilo ndilo linalowafanya wanawake wafanye hivyo. Hilo ndilo linalowafanya wahubiri wafanye hivyo. Wanamshughulikia askofu badala ya Yesu. Wanashughulikia hilo, ninii yao—mfuko wao wa fedha, kusanyiko kubwa

¹⁷² Hebu angalia tu kama mimi ninapendwa sana na watu. Wachukue watu, wanaotoka nje ya Jeffersonville, pamoja na kundi dogo lililopo hapa linalotoka Jeffersonville; hebu chukua watu kutoka nje, ya Jeffersonville, kutoka katika Maskani hii asubuhi ya leo, nisingekuwa ama kupata nusu dazeni wa kuhubiria. Ni kitu gani? Lina washiriki wa kutoka kila mahali nchini; kutoka New York, kutoka Massachusettes, hadi Boston, Maine, Tennessee, Georgia, Alabama, na kote nchini. Wanakusanyika pamoja. Amina! Hivyo ndivyo Yeye alivyosema. “Itakuwa Nuru yapata wakati wa jioni.”

¹⁷³ Hawawezi kutambua Nuru ya jioni. Hiyo ndiyo shida. Haliitambui kamwe. Limekuwa kipofu sana. Biblia ilisema alikuwa ni kipofu.

¹⁷⁴ Urusi ilichukua tu mahali pake ulimwenguni, katika sayansi, si zaidi ya karibu miaka arobaini iliyopita. Mnajua, wakati Vita vya Kwanza vya Dunia vilipotokea, wao kamwe... Waliipuuza Urusi. Ndugu Roy... Ilikuwa tu ni kundi la baradhuli, maskini Wasaiberia wakubwa, wenye mandevu usoni mwote, na hawakujua mkono wa kulia wala wa kushoto. Hiyo ni kweli, Urusi, bali ilitambua mahali pake. Ilibidi ifanye hivyo kuyatimiza Maandiko. Mnajua unabii wangu wa yale niliyosema yatatukia, jinsi hizo zote zingejikusanya katika ukomunisti. Sasa inauongoza ulimwengu katika sayansi. Tuko mbali sana nyuma yake. Wengine wote ulimwenguni wako nyuma yake. Inashikilia nafasi yake ya uongozi. Ilitambua tu ya kwamba ilikuwa na akili, pia.

¹⁷⁵ Angalia, mwanadamu ana hisi zile zile sita alizokuwa nazo miaka elfu sita iliyopita. Miaka elfu sita iliyopita, kwa hisi alizokuwa nazo, aliwasiliana na makazi yake ya duniani na kumtumikia Mungu. Na sasa, katika miaka sabini na mitano iliyopita, mwanadamu ametoka kutoka kwenye magari ya farasi, akafikia mwanaanga. Kwa nini? Aliondoa imani yake kwa Mungu, akaiielekeza kwenye hisi zake na uwezo wake kama mwanadamu. Mling'amua jambo hilo? Aliacha kumtumainia Mungu. Yeye anajiamini mwenyewe.

¹⁷⁶ Kama huyu mwanamke kafiri. Jina lake ni nani, kule Washington, aliyebadilisha haya yote? [Mtu fulani anasema, "Murray."—Mh.] Ati jina lake ni nani? ["Murray."] Murray, alisema, "Mradi tu tuna jeshi la nchi kavu na la majini, hatumhitaji Yehova wa kale." A-ha. Sijali tuna nini.

Kwangu mimi, ni Yehova ama sitaki chochote. Acha jeshi la nchi kavu na la baharini lizame, na litazama, bali Yehova atadumu milele. Mradi tu mimi ni sehemu Yake, na ni Mwanawe, nitadumu Naye milele; si kwa wito wangu wala kwa uchaguzi wangu, bali ni kwa uchaguzi Wake. Amina, amina! Sikuwa na uhusiano wowote nalo. Yeye Ndiye anayehusika! Nipe Yeye ama unipe mauti. Acha mataifa yainuke na kuanguka; Yehova atadumu. Yeye amefanya jambo hilo, katika nyakati zote; wakati Rumi ilipoanguka, wakati Misri ilipoanguka, na hayo mengine yote yalipoanguka. Naye angali anadumu kuwa Yehova. Loo, haleluya! Ninajisikia wa kidini.

¹⁷⁷ Sababu ya Urusi kuzinduka, ilipaswa izinduke. Ni kama tu vile ambavyo ilibidi Israeli warudi kwenye nchi ya uenyeyi wao. Ilibidi Mungu awafukuze Israeli warudi kwenye nchi yao, kwa ajili ya zile Baragumu. Na vivyo hivyo ilimbidi Mungu aipeleke Urusi juu kule, katika ukomunisti, ipate kufanya yale hasa ambayo ilitabiriwa itafanya.

¹⁷⁸ Mwanadamu na hisi zake sita alikuwa ndiyo kwanza aje, farasi na gari lake, akimtumainia Mungu. Katika miaka sabini na mitano iliyopita, aliacha kumtumainia Mungu. Wakati walipoidhinisha katiba ya Marekani hii, walimweka Mungu katika kila jambo walilofanya. Sasa hata hawana mkutano, wala hata hawalitaji Jina Lake. Hiyo ni kweli. Wanategemea kiburi chao cha sayansi yao, wao, ujanja wao wa sayansi yao; ama lile kundi la ufisadi. Hiyo ni kweli kabisa. Ulimwengu mzima umemezwa katika kutoifahamu Biblia. Bi- . . . ulimwengu mzima umemwacha Mungu.

Lakini, hebu wazia tu, papo hapo katikati ya hayo yote, na madhehebu ya kanisa na ufisadi wao wote wa seminari na kila kitu, Mungu amechukua Neno la manabii Wake na kumbangua Bibi-arusi ambaye ataamini. Alisema atafanya jambo hilo. Amekata kutoka katika kitu hicho kile alichohidi atafanya.

¹⁷⁹ Wao wanategemea akili zao za kibinadamu, sayansi yao ya kibinadamu, na kadhalika; walimwacha Mungu, ambaye wakati mmoja alimwamini. Marekani imemwacha Mungu. Hata walimfukuza shuleni, kwa maana watoto wetu wadogo hata hawawezi kusikia habari Zake. Walimfukuza shuleni. Sasa wanajaribu kumwodoa kwenye dola, “Tunamtumaini Mungu.” Watayaondoa maandishi yale katika kiapo cha kuitii bendera, “Taifa moja chini ya Mungu.” Watayaondoa hayo.

¹⁸⁰ Unaona, wameenda kwa hisia zao wenyewe na hisia zao wenyewe. Kwa sababu, katika miaka sabini na mitano iliyopita, yeye hajabadilika hata kidogo katika hisia zake, yeye angali ni mtu yule yule aliyumbwa na Mungu hapo mwanzo.

Lakini, katika siku hizi za mwisho, je! hamwezi kutambua mahali tulipo? Na kanisa limegeuka, kutoka kwa Mungu, kuenda kitu hicho, kwenye ujuzi wa kiseminari, na kadhalika, badala ya Neno. Hata hawamtambui katika mikutano yao, katika shule zao, wala chochote kile, tena.

¹⁸¹ Israeli, katika miaka ishirini na mitano iliyopita, imetambua kitu fulani kimewaleta kwenye nchi ya uenyeji wao, kama ilivyoahidiwa. Hawajui jinsi jambo hilo lilivyofanyika. Waliteseka kama chochote kile, ufia imani, chini ya hizo Baragumu, bali wako katika nchi ya uenyeji wao. Hawajui ni kwa nini.

¹⁸² Kwa nini Urusi ilizinduka? Kwa nini mataifa yalizinduka? Kwa nini mwanadamu ameweza kufanikiwa? Wakati wanasayansi, miaka mia tatu iliyopita, mwanasayansi mmoja wa Kifaransa alifingirisha mpira katika mwendo fulani ardhini, na kuthibitisha, kwa utafiti wa sayansi, “Kama mtu akifanikiwa kamwe kusafiri kwa mwendo wa kasi sana wa maili thelathini kwa saa, nguvu za uvutano zitamwondoa duniani; kwa kadiri ya uzito wake, kwa kadiri ya uzito wa mpira huo.” Sasa anaenda maili elfu kumi na saba kwa saa, unaona, angali anajitahidi kupanda juu. Ndio kwanza atambue jambo hilo, juzi juzi. Ni kwa nini? Inabidi kuwa hivyo.

¹⁸³ Mbona, kanisa lilikuwa likisimama kwenye mwamba wa Yesu Kristo. Haidhuru mtu yeyote alisema nini, walidumu moja kwa moja pamoja na Neno hilo, Ujumbe wa wakati; Luther, Wesley, na kote kupita kule. Na sasa wanayageukia mapokeo. Ni kwa nini limefanya jambo hilo?

¹⁸⁴ Miaka ishirini na mitano iliyopita, Israeli ndiyo kwanza itambue ya kwamba wako kwenye nchi ya uenyeji wao kwa ajili ya jambo fulani. Ilitabiriwa itawabidi kukusanyika tena; Hosea alisema hivyo. Tulilisoma muda mchache uliopita. Mungu na atusaidie kufahamu jambo hilo! Vema.

¹⁸⁵ Wakati huo huo, Bibi-arusi ametambua Nuru ya jioni, ndio kwanza aanze kutambua. Wapentekoste wenye njaa wameanza kutambua ya kwamba madhehebu hayo hayana

vitu walivyokuwa wakitafuta, wamechanganyikiwa sana na kutengana. Unaona, ni wakati wa kutambua, kutambua. Inakupasa kutambua.

Ulimwengu umetambua. Mataifa yametambua. Sayansi imetambua. Ibilisi ametambua ni wakati ambapo anaweza kuwaharibu wanawake, kuliharibu kanisa, kuwaharibu watu. Ametambua jambo hilo.

Naye Mungu ametambua ya kwamba kuna watu fulani ulimwenguni ambao aliwakusudia Uzima. Ametambua huu ndio wakati wa kutuma Ujumbe Wake. Ameutuma. Watu wametambua jambo Hilo, wakati wa Bibi-arusi umetambua Nuru ya jioni.

¹⁸⁶ Laiti Sodoma ungalizitambua siku zake, wakati ulipoona hao wajumbe wakishuka kwenda kule, kama vile Billy Graham na Oral Roberts!

¹⁸⁷ Sasa, fisadi fulani huko Phoenix ndio kwanza aibuke na kusema... akacheza sehemu hiyo ya ka—kanda, na kusema nilisema hapa, mimi “sina budi kubatizwa katika Jina la Yesu,” kasema hivyo. Na kisha akasema, “Sasa unaona *hapa*, hapa yeye alisema...” Nilipokuwa nikizungumza kuhusu Afrika, jinsi walivyobatiza mara tatu kifudifudi, na kichalichali. Kasema nilisema, “Haileti tofauti yoyote.” Unaona, yeye hakucheza kanda yote; ni sehemu hiyo tu, kisha akaifunga.

Ambapo, lingekuwa ni kosa lipaswalo afungwe jela kwa kufanya hivyo. Kanda hizo zina uwakala mkamilifu. Hakuna mtu anayeweza kuzichezea. Afadhali usizichezee. U—u—utashitakiwa na sheria. Lakini je! tungeweza kufanya hivyo? La. Yeye alisema, “Waacheni.” Mungu aliniambia yale yatakayotendeka. Angalieni tu, mwangalieni tu mtu huyo. Unaona?

¹⁸⁸ Wakati uo huo, Bibi-arusi ametambua Nuru ya jioni.

Laiti Sodoma ungaliitambua saa yao!

¹⁸⁹ Sasa, mtu yuyu huyu alicheza kanda, kasema, “Angalieni hapa, ninyi Wapentekoste,” kasema, “nanyi Wabaptisti. Mtu huyu, nabii wa uongo, William Branham,” unaona, “amesema ya kwamba Oral Roberts na Billy Graham walikuwa Sodoma.” Unaona, kisha akafunga hiyo kanda; hivyo tu, unaona.

Asingeendelea mbele kusema, kwamba, “Walikuwa ni wajumbe wa Sodoma.” Si kwamba wako Sodoma, “Walikuwa kule kama mjumbe wa Sodoma.” Mtu yeyote anajua nilisema hivyo. Cheza kanda yako.

“Yeyote atakayeondoa au kuongeza kwake, huyo ataondolewa sehemu yake.” Ni Neno la Bwana. Linadumu hivyo.

¹⁹⁰ “Kama Sodoma ungalimtambua mjumbe wake, ungalikuwa unasimama leo,” Yesu alisema, kama ungalitambua jinsi vile ambavyo Ibrahimu alitambua.

Ibrahimu alijua kulikuwa na mwana wa ahadi aliyekuwa anakuja. Lakini alijua ilibidi kuwe na badiliko fulani kwa njia fulani, kwa kuwa alikuwa ni mzee sana, na Sara pia. Lakini alipomwona huyo Mtu ambaye aliweza kutambua siri za Sara, akiwa nyuma Yake, yeye alitambua ile saa aliyokuwa anaishi. Akasema, “Bwana wangu, hebu niwalettee maji kidogo hapa mnawe miguu Yenu.” Wakala kipande cha mkate. “Hebu nikushihi, kaeni muda kidogo zaidi,” unaona, hapa, “B-w-a-n-a wangu,” herufi kubwa B-w-a-n-a, “Elohim.” Yeye alitambua ya kwamba Mungu alikuwa akisema naye katika mwili wa kibinadamu. Alitambua ishara yake, na akabarikiwa na Bwana.

Sodoma hawakutambua siku yao, nao wakachomwa moto. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku ile, ndivyo itakavyokuwa wakati Mwana wa Mungu ana . . . ama Mwana wa Adamu atakapodhihirishwa.”

¹⁹¹ Sasa, kanisa halijaitambua siku yake. Kama vile Israeli, ilivyolazimishwa kurudi Palestina, litalazimishwa kuingia katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Kwa nini? Halikutambua saa yake. “Enyi watu, tokeni kwake, msishiriki dhambi yake!” Kimbieni, kwa ajili ya maisha yenu, la sivyo mtashikwa mkiwa na alama ya mnyama wala hamwezi kufanya lolote juu yake.

“Yeye aliye mchafu na azidi kuwa mchafu. Yeye aliye mtakatifu,” si *atakayekuwa* mtakatifu, “mtakatifu sasa hivi. Yeye aliye mtakatifu,” si aliyeka . . . mwanawake aliyekata nywele zake; hawezi kuwa mtakatifu. Sasa, hilo linasikika kali sana, bali hayo ni Maandiko. Biblia inasema, “Yeye yuaibisha kichwa chake,” na kichwa chake ni mumewe. Kichwa cha mumewe ni Kristo, kwa hiyo yeye anamwaibisha Kristo. Anawezaje kuwa “asiyeheshimika” na asiwe “mchafu”? “Yeye aliyekata nywele zake na azidumishe hivyo. Yeye, yeye anayevaa kaptura aendelee kuzivaa. Yeye anayekana Neno na aendelee kulikana.”

“Bali yeye aliye mtakatifu na azidi kutakaswa. Yeye aliye mwenye haki na azidi kufanya haki; Neno safi la Mungu, Mwana wa Mungu aliyedhihirishwa. Azidi kutakaswa, azidi kufanya haki!” Kutambua! Naam, bwana! Siku si . . .

Kanisa halijaitambua siku yake.

¹⁹² Kama vile Israeli, waliporudi kwenye nchi yao ya ahadi, hawajui jinsi walivyorudi kule. Walirudishwa tu moja kwa moja kule. Kwa nini? Nguvu za kitaifa zilimweka nchini mwake.

Sasa nitasema jambo fulani. Nguvu za kitaifa ziliwaweka Israeli katika nchi ya uenyeji wao; nguvu za kitaifa zitaliweka kanisa katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni; bali nguvu

za Mungu zitawaweka watu katika Bibi-arusi. Ulimwengu unalazimisha *huku*, na ulimwengu unalazimisha *kule*, bali Mungu analazimisha kupanda juu. Roho wa Mungu, ambaye ni Neno la Mungu, “Neno Langu ni Roho na Uzima,” litamweka Bibi-arusi mahali Pake. Kwa maana, Yeye Atatambua nafasi yake katika Neno, ndipo anakuwa ndani ya Kristo, litamweka kwenye nafasi yake. Hakuna nguvu za kitaifa zitakazofanya jambo hilo. Bali nguvu za kitaifa ziliwasukuma Israeli zikawapeleka katika nchi ya uenyeji wao; nguvu za kitaifa za Baraza la Makanisa zitaingiza kila madhehebu ndani yake; bali Nguvu za Mungu zitamwinua Bibi-arusi zimpeleke Utukufuni, kutoka kwake.

¹⁹³ Loo, enyi watu, itambueni siku yenu, kama Yesu alivyowaonya; ile ishara ya Sodoma, na hali za kanisa la siku hizi.

¹⁹⁴ Angalia yale Yeye aliyosema yatatukia katika siku hii. Yasikilizeni kwa makini sana. Ishara ya Sodoma itatukia katika siku hii; ishara kama Ibrahimu, siku ile kabla ya Sodoma, aliyeitwa atoke. Mambo yote haya yaliyotabiriwa, yatakuwa yakitukia sasa. Angalia siku unayoishi. Tumelipitia jambo hilo tena na tena.

¹⁹⁵ Sasa Yeye amewaahidi kuwatumieni Nuru ya Mbinguni, kuivisha Neno Mbegu ambalo lingepandwa kwa ajili ya siku hii. Mbegu hiyo imo *Humu* ndani. Mbegu hiyo ni Biblia. Mbona? Yesu alisema hivyo. “Neno ni Mbegu ambayo mpanzi alipanda.”

Na, sasa, kabla hujapata mazao yoyote, haidhuru kama ukiipanda hiyo mbegu, haina budi kupata nuru ya kuivisha mbegu hiyo, la siyvo itaoza wala haitafaa kitu; itaangamia. Bali kama ina mbegu ardhini, ardhi nzuri, ikiangaziwa nuru ya jua ipaswavyo, haina budi kuiva.

Naye aliahidi ya kwamba katika siku za mwisho, katika wakati wa jioni, Mwana angechomoza apate kuivisha Mbegu hiyo. Mbegu inahubiriwa. Mwana wa Mungu anaivisha Mbegu hiyo, kwa kuthibitisha, akiifanya ichipuke mbele yenu na kuthibitisha ya kwamba ni ya kweli. Je! mnalipata jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Itambue siku yako.

Ninafunga sasa. Sasa ni wakati wa kufunga.

¹⁹⁶ Na Laodikia tajiri, kipofu, yenye elimu, wangeliondoa Neno katikati yao. Je! wamefanya hivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Alisema wangefanya hivyo.

Kama vile wale manabii wa zamani walivyotumwa kuthibitisha Neno lililoahidiwa la siku yao, ili kwamba watu waliokusudiwa, siku yao, waliliona Hilo. Kama vile yule mwanamke pale kisimani, kama vile Nathani, kama vile kipofu Bartimayo, kama vile Petro, na hao wengine waliotambua jambo Hilo. Yeye alikuwa ndiye hilo Neno. Na matokeo, “Nisipozitenda kazi ambazo Baba aliahidi ningezifanya, basi msiniamini Mimi.

Bali kama nikizitenda kazi hizo, ingawa hamniamini Mimi, aminini kazi hizo. Zinawaambia Mimi ni Nani.” Mnalipata? Vema, msikose hiyo siku, aliyotumwa. Wanaume na wanawake wa siku zingine waliitambua, nao wakaingia na walikuwa salama.

¹⁹⁷ Wapentekoste, loo, jamani, kwa nini hamwitambui siku yenu? Itambueni siku ya wakati wa jioni. Iko hapa, na iko hapa, hiyo, kuthibitisha kule kuja kwa Kristo, kuithibitisha. Tuko mwishoni. Itambueni siku yenu.

¹⁹⁸ Ninajua nimewaweka kwa muda mrefu. Ni saa sita sasa. Lakini, ninapenda Chakula hiki, Hiki ni Uzima. Ni Uzima. Ni Uzima, kwa mwaminio. Itambue siku unayoishi, na ishara ya wakati wake.

¹⁹⁹ Angalia mahali kila kitu kilipo: Israeli; mahali kanisa lilipo; wazinzi walipo; mahali Bibi-arusi amesimama. Kumbakia nini? Kitu kinachofuata, ni kutwaliwa juu kwa Bibi-arusi. Bila shaka, kila kanisa linatarajia jambo kuu. Wapentekoste wanasema, “Utukufu kwa Mungu! Itakuja siku ambapo watafanya *hivi*, na watafanya *vile*.” Unaona, wao ni watangaza imani. Wanaamini.

²⁰⁰ Kama vile, wakati mmoja, Kayafa alivyosema, “Je! si yafaa kwamba mtu mmoja afe, wala taifa lote lisiangamie?” Yeye alikuwa kuhani mkuu, Biblia ilisema, sababu ya yeye kusema hivyo. Alitabiri, bila kujua alilokuwa akisema. Bali je! alitambua ukweli halisi wa jambo hilo, kwamba alikuwa akimtoa dhabihu Mungu yule aliyedai kwamba yeye ni kuhani mkuu Wake?

Ndivyo ilivyo, leo hii! Wao wanatazamia, huko ng’ambo mahali fulani, wa—wakati mkuu uje.

²⁰¹ Mbona, ninahudhuria mkutano wa Wafanyabiashara pamoja nao. Wanasema, “Utukufu kwa Mungu!” Hao wahubiri wanaamka tu na kuuchochea umati, na kusema, “Kuna ufufuo mkubwa unaokuja. Mkono wa Bwana utakuwa juu ya nchi!” Na jinsi watu wanavyoenda, wakikimbia kama... Wala hawatambui huo uko chini ya Baragumu za Israeli. Kwa nini wanafanya jambo hilo? Ni kwa sababu wao wanakiri kwamba ni Wakristo, wala hawatambui. Wala Kayafa hakutambua yale aliyokuwa akifanya. Wala watu hawatambui kwamba wanaukataa ule Ujumbe hasa waliotumiwa. Amina!

²⁰² Kila sehemu ya Maandiko, tumeipitia siku baada ya siku, na juma baada ya juma, mpaka ni Kweli isiyokanushika. “Kama vipofu hawawezi kuupokea,” Yesu alisema, “waacheni. Kipofu akimwongoza kipofu mwenziwe, wote wataanguka shimoni.” Sijui ni lini, sijui ni wapi, bali ninajua inakuja.

²⁰³ Unajua, ninaona ni kwa nini Shetani hakutaka nifanye jambo hili. Jana, nilijisikia vibaya sana. Nisingeweza kupata Neno lolote kutoka kwa Bwana. Nilifanya kila kitu nilichojua jinsi ya kufanya, wala sikuweza. Na asubuhi ya leo,

nilipoamka... Nilikula mahindi kidogo, jana, na yalionekana kama yalika tu mle ndani ya tumbo langu. Nilikuwa mgonjwa sana, ilikuwa tu—ilikuwa tu ni vigumu kwangu kupata kitu. Nikawaza, “Hivi kuna nini? Ninashuka kwenda kule, wala sijui ninaloenda kusema. Na, Bwana, hata siwezi kupata Andiko moyoni mwangu, kuliandika. Siwezi kupata kitu.” Kamwe sikujua la kufanya.

Basi, baada ya Ujumbe kuanza kunijia, Shetani aliendelea kusema, “Unajisikia vibaya sana. Kichwa chako kinauma. Wewe ni mgonjwa. Huwezi kushuka kwenda kule. Huwezi kusimama pale. Itakuwa *hivi*, itakuwa *vile*.”

204 Ninakumbuka, wakati mmoja, hadithi fulani ya maskini mkukni mmoja huko Uingereza. Alikuwa ni mtu wa kawaida tu. Nao walisema ya kwamba m—m—mfalme, mmoja wa hao wafalme katika siku za mwanzoni alikuwa akienda kwenye ikulu ya—yake. Na, huyu, hakuwa na mtu... Alikuwa na ujumbe aliokuwa akitaka kuupeleka, ujumbe wa haraka, kwa sababu ya adui. Na kwa hiyo a—a—akamwambia maskini jamaa huyu aliyekuwa amesimama pale, akasema, “Hapa, chukua ujumbe huu, chukua ujumbe huu! Kimbia uende mahali—mahali *fulani*, na uamuru jambo *hili* lifanywe.” Naye akasema, “Chukua fimbo yangu ya kifalme mkononi mwako. Hiyo itakuthibitisha, ya kwamba mimi ni... umetumwa kutoka kwangu mimi.”

205 Naye akautia kwenye joho lake, na huyoo akaenda zake. Walinzi kila mahali wakimsimamisha, kila mtu. Akipaza sauti, “Ondoka njiani! nina ujumbe wa mfalme.” Amina. “Mimi ni mjumbe wa mfalme,” neno lililothibitishwa.

206 Nikawazia, “Shetani, ondoka njiani! Nina Ujumbe wa Mfalme. Sina budi kwenda.”

207 Wakati mmoja walipomwua Mfalme wa Amani, na kumweka kaburini, kisha wakalitia kaburi muhuri, na mauti yakamshikilia siku tatu usiku na mchana. Lakini kwenye asubuhi ya Pasaka Yeye alishika fimbo ya mfalme mkononi Mwake, na akapaza sauti, “Ondoka njiani, ewe mauti! Ondoka njiani, ewe kaburi! Funguka! Mimi ndiye Ujumbe wa Mfalme. Lazima nitoke nije nikathibitishe ufufuo huu. Mimi Ndimi ufufuo na Uzima.” Haleluya! Ninajisikia mwenye furaha sana sasa.

Ni Ujumbe wa Mfalme. Hebu na tuutambue, wapendwa, kwa kuwa tumeitwa kukusanyika pamoja kwa ajili ya kupigwa kwa Baragumu. “Kwa maana Baragumu ya Bwana Italia, ndipo hakutakuwa na wakati baada ya hayo.”

208 Yeye amewakusanya Israeli. Zile siku tatu, katika siku ya tatu Yeye alisema angewakusanya. Miaka elfu mbili na mia saba imepita. Katika siku hiyo ya tatu Yeye alisema angewakusanya pamoja, naye amefanya hivyo. Yeye alisema angetufahamisha njia ya Uzima. Hiyo hapo, anangojea tu Bibi-arusi aondoke

njiani ili wale wapate kuja, wale manabii wawili, manabii wa Kiebrania, ambao wao watawatambua.

²⁰⁹ Mnakumbuka wakati ule nilipotua Cairo, nipate kwenda kule, wakati Lewi Pethrus aliposema, “Ndugu Branham, kama wakipata kuona hilo . . . Wao wanaamini manabii wao.”

²¹⁰ Nikasema, “Ni jambo zuri kwangu.” Unaona jinsi mwanadamu alivyo? Lakini unaona neema ya Mungu? Nikasema, “Nitasoma Agano hili Jipya.” Wao wanalisoma. Lewi aliwatumia, zaidi ya milioni moja, kule. Ndugu Lewi Pethrus kutoka Sweden. Wangeisoma, wakija huku na huku kule, hao Wayahudi; si kama kundi hili la kisasa la Wayahudi, bali katika nchi ya uenyeji wao. Ndipo wakaja, wakasema, “Kama huyu ndiye Masihi, hebu na tumwone akifanya ishara ya nabii, tutaamini.”

²¹¹ Lewis Pethrus akasema, “Ndugu Branham, hiyo hapo nafasi. Hiyo hapo nafasi. Mtu mmoja aliniambia hivyo, kwamba hiyo ingekuwa ni nafasi. Niliipata sawa sawa tu moja kwa moja.”

Mtu mmoja akaja na kuketi pale, Ndugu Arganbright, akasema, “Ndugu Branham, hiyo ingewashitua sana Israeli! Walete mbele Yake, na uwaonyeshe ishara ya nabii. Wataiamini.”

²¹² Nikasema, “Bwana, mimi huyu hapa, niko tayari.” Nikaruka nikaingia kwenye ndege; nikachukua pesa nikajinunulia tikiti; nikasimama huko Cairo. Kasema, “Naam, niko tayari.”

²¹³ Roho Mtakatifu akasema, “Hapa si mahali pako. Huu sio wakati wako.” Unaona, unajitangulia. Nikawazia, “Loo, jamani! Nimekuja umbali wote huu; ni—nitaenda.”

²¹⁴ Kitu fulani kikasema, “Ishia papa hapa! Usiende kule. Geuka uende India. Usiende huko. Nenda India, bali usiende hapa.”

²¹⁵ Nikawaza, “Kwa nini?” Nilipokuwa nikiondoka kwenda nyuma ya banda la ndege, nikasema, “Bwana Yesu, hii ina maana gani?”

Ndipo akanijulisha. “Si Mmataifa. Ni hawa manabii.” Haina budi kulingana na Maandiko. “Inawapasa Musa na Eliya kuja.” Na, isitoshe, Bibi-arusi hajaondolewa njiani bado. “Na hao manabii watarudi nao watafanya ishara ya nabii.” Hayo ni Maandiko. Hapo yote yametimizwa basi, kikamilifu, Israeli kama taifa itazaliwa katika siku moja. Amina! Nuru za jioni zinaangaza!

Kutakuwa na Nuru kwenye wakati wa jioni,
Njia ya Utukufuni hakika mtaipata;
Katika njia ya maji ndiko kwenye Nuru leo,
Kuzikwa katika Jina la thamani la Yesu.

Vijana kwa wazee, tubieni dhambi yenu yote,
 Roho Mtakatifu hakika ataingia;
 Nuru za jioni zimekuja,
 Ni kweli kwamba Mungu na Kristo ni Mmoja.

²¹⁶ Tuko katika wakati wa mwisho, mpendwa. Na ndipo tunafikiri juu ya wimbo huu wa mwandishi aliyevuviwa, wakati aliposema:

Mataifa yanavunjika, (hii ni kama miaka kumi
 na tano iliyopita), Israeli inaamka,
 Ishara ambazo manabii walitabiri;
 Siku za Mataifa zimehesabiwa, (angalia
 uchafu wake sasa) zimekumbwa na hofu;
 Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu.
 Siku ya Ukombozi imekaribia,
 Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
 Jazweni na Roho wa Mungu, zitengenezeni na
 kuzisafisha taa zenu,
 Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia.
 (Hiyo ni kweli.)

Manabii wa uongo wanadanganya, Ukweli wa
 Mungu wanaukana, (je! si ni kweli!)
 Yesu aliye Kristo ndiye Mungu wetu.

Hawaamini jambo Hilo. Wana kila namna ya itikadi na mambo kadha wa kadha!...?...kweli. Bali nabii alisema... Ama, yule mwandishi aliyevuviwa alisema:

Tutatembea pale ambapo mitume
 wamekanyaga.

²¹⁷ Mnakumbuka katika ono langu? Nilisema, “Kama watu wa Paulo wakiingia, vivyo hivyo na wangu pia, kwa kuwa nilifanya kabisa vile vile yeye alivyofanya.” Ninadumu moja kwa moja Nalo.

Hao mamilioni wakatupa mikono yao, wakisema, “Tunategemea jambo hilo!”

Ni nini? Tambueni siku tunayoishi, wakati tunaoishi, ishara ya wakati tunaoishi. Huenda ikawa muda umeenda sana kuliko tunavyofikiri. Moja ya siku hizi, yeye aliye nje na azidi kukaa nje. Yeye aliye ndani ni sharti akae ndani milele. Mlango utafungwa.

²¹⁸ Kama kuna baadhi hapa asubuhi ya leo ambao bado hawajaingia ndani, loo, katika Jina la Yesu, watu wangu wapendwa...

Usimwangelie huyu mtumishi asiye na elimu anayesimama hapa, asiyejua kusoma, asiye na maarifa, asiye na kisomo; usiangalie jambo hilo. Bali angalia Neno linalothibitishwa. Mwangalie Roho Mtakatifu mkuu Ambaye anathibitisha jambo Hilo kwamba ni Kweli. Tuko katika wakati wa jioni. Muda umepitiliza sana kuliko unavyofikiria. Usininii...

²¹⁹ Enyi wanawake, acheni nywele zenu zikue. Ewe dada, tafadhali toa hizo nguo chafu. Tupilieni mbali hizo sigara. Kwa maana saa itakuja, ambapo, “Yeye aliye mchafu, na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki, na azidi kufanya haki. Yeye aliye ndani yuko ndani; yeye aliye nje yuko nje.” Ile nafasi ndogo sana, ya pembeni, “Kama ni vigumu kwa mwenye haki kuokolewa, mwenye dhambi na asiye mcha Mungu atakuwa wapi,” anayekana Ukweli, mwajua, “wataonekana wapi?”

Na tuinamishe vichwa vyetu.

²²⁰ Sasa, katika Nuru ya wakati huu tunaishi, Nuru ya siku tunayoishi sasa; enyi watu wa thamani na wapendwa, ninyi mnaotoka katika mikoa mbalimbali kote nchini, hebu na tuninii sasa, na mimi pamoja nanyi, kwenye madhabahu hii, hebu na tujichunguze. Roho wa Mungu mioyoni mwetu yukoje leo? Kumbuka, ni Roho yule, ambaye hahukumiwi, hatiwi unajisi; fundisho lolote la kanisa, na kila kitu, kimeondoka kabisa.

²²¹ Usingethubutu, kujaribu kuongeza kwenye Hilo wala kuondoa Kwake. Kwa kuwa, kama ukijaribu kuweka tafsiri Kwake, wewe mwenyewe, sehemu yako inaondolewa kwenye Kitabu cha Uzima. Je! unajaribu kusema jambo fulani ambalo Roho hajasema? Je! unajaribu kumfanya asikike kama alisema jambo fulani? Ama, unalichukua vile lilivyosema hasa, na kuliacha namna hiyo? Je! unaunganisha, unakata, unarekodi, kufanya mabaya? Je! umefanya hivyo?

²²² Unasema, “Vema, sijisikii kama ninapaswa kufanya jambo *hili*. Ama, labda, na—na—najua kanisa langu haliliamini hilo. ‘Hilo ni neno la mtu mmoja tu kuhusu Hilo.’”

Mtu mmoja huyo ni Mungu. Biblia hapa inasema hupaswi kukata nywele zako. Hizi...Biblia ilisema jambo hilo. “Itakuwa kwamba wanawake watavaa mavazi kama ya mwanamume, na jinsi wangukuwa ni chukizo kwa Mungu.” Jinsi Roho Mtakatifu alivyonena kupitia kwake, chombo hiki kinyenyekevu, kisichostahili, ambacho ilitokea tu kwamba kilikuwa kimesimama wakati ambao yule Mfalme mkuu alisema, “Hii hapa fimbo Yangu ya kifalme, Neno Langu.” (“Hii hapa Fimbo Yangu ya kifalme,” hasa.) “Chukua Fimbo Yangu ya kifalme, uende zako, na uupeleke Ujumbe.”

²²³ Ninajua madhehebu yalijaribu kuukomesha, na kuukataa, na kuutupilia mbali, na kuupiga mateke, na kila kitu. Lakini, kwa neema ya Mungu, naenda zangu, nikipiga makelele toka taifa hadi taifa, mahali mahali, toka kanisa hadi kanisa, “Tokeni kwake!” Haupendwi na watu, bali ni wa Kweli.

²²⁴ Je! mtaupokea katika—katika—Roho iliyoundika? Je! mtaupokea katika Roho uliotolewa? Kama ninyi bado. . . Hatuna nafasi kwa madhabahu; moyo wako ndio madhabahu. Tafadhali inua mkono wako, useme, “Mungu, unirehemu. Mruhusu Roho wa Mungu aje ndani yangu, akinihukumu sasa kwa dhambi

zangu zote, na kuvunjika moyo kwangu, tabia zangu zote mbaya, na hasira kali, na fujo, na kupigana, na hamaki, na kila kitu ambacho nimekuwa nacho. Nami ninajua jambo fulani, ya kwamba Roho yangu si laini na tamu kwa ajili ya Mbinguni. Nifanye laini, Bwana, katika majira haya ya mwisho. Huenda haya yakawa ndiyo mahubiri ya mwisho nitakayowahi kusikia. Huenda huu ukawa ndio wakati wa mwisho nitakaowahi kusikia Ujumbe. Ninainua mkono wangu. Mungu, nirehemu.”

225 Mungu awabariki. Mikono dazani nyingi. Sasa, kwa muda kidogo tu wa maombi ya kimyakimya kwa ajili yenu. Wewe uliyeinua mkono wako, inaonyesha ungali unapenda. Inaonekana kwangu kana kwamba Roho angali anamwita mtu fulani.

226 Mungu mpendwa, Wewe unayejua mambo yote. Nawe ulifanya vitu vyote kwa kusudi la vitu vyote, kwa kuwa, wengine walipaswa kuhukumiwa, wengine walipaswa kupofushwa; wengine, “kama mfinyanzi aliyeumba chombo,” kama Paulo alivyosema, “kimoja kwa heshima na kingine kwa aibu.” Kile kilichotengenezwa kwa ajili ya aibu, kilikuwa tu kionyeshe kile kilichotengenezwa kwa heshima. Lakini je! haliko kwenye mkono wa Mfinyanzi kufanya vile atakavyo? Je! haliko kwenye mpango wa Mungu uliokusudiwa, kuita? “Yeye aliyemjua tangu zamani, alimwita. Hao aliowaita, aliwahesabia haki. Na wale aliowahesabia haki, aliwatukuza.”

227 Huenda ikawa wengine wao hapa leo ni kama maskini mwanamke yule pale kisimani, wametoka kwenye uchafu, wametoka kwenye kutokuamini, wametoka katika mapokeo ya mwanadamu, mafundisho yaliyobuniwa na wanadamu. Pengine ni mara ya kwanza wamepata kusikia mambo haya, lakini kitu fulani kimeonya mioyo yao kiajabu. Kuna mikono mingi, mingi iliyoinuliwa, Bwana. Jalia yule Mfinyanzi mkuu akitwae chombo hicho sasa na akifinyange akifanye chombo cha heshima. Ninaamini kuna sababu fulani, Bwana, la sivyo wasingekuwa wakifanya jambo hilo, wasingekuwa wakisema jambo hilo. Ningali ninaamini, ninashikilia kwa ajili yao.

228 Jalia mtumishi Wako mnyenyekevu asihi, Bwana. Jalia tusihi kwa ajili yao, kama mtu anayesimama kati ya walio hai na waliokufa; kama yule huko Sodoma aliyekuwa akisihi kwa ajili ya Wasodoma, “Tokeni kwake! Tokeni kwake, upesi!”

229 Naomba waje, Bwana, kwa unyenyekevu na utamu kwenye kiti cha enzi cha Mungu sasa, moyoni mwao, wakisema, “Yesu, tangu leo, na kuendelea, Wewe utakuwa ni wangu. Ninatoa ahadi hii Kwako sasa hapa, ninapoketi hapa katika kiti hiki ambapo Roho Wako amenigusa. Kama Yeye amenigusia hapa, sina haja ya kwenda mbali zaidi na mahali papa hapa. Papa hapa ndipo ulipokutana nami; papa hapa ndipo tutakapoyamalizia; papa hapa kwenye kiti hiki cha pili, kiti cha tatu, kiti cha tano,

popote pale. Papa hapa ndipo litakapotatuliwa, maana hapa ndipo uliponihukumia, na hapa ndipo uliahidi kutatua jambo hilo. Kwa kuwa ingawa ningekuwa mchafu na mwenye kinyaa, nitafanywa mweupe kama theluji. Nitaamini Neno Lako lote. Niko tayari kutembea ndani Yake, kuliadini, kulikubali.

“Na sasa ninatenda hili kwa utukufu wa Mungu, nikijua ya kwamba maisha yangu hayanifai, hayafai mbele za Mungu, hayafai kwa jirani zangu, hayafai kwa kitu kinginecho; ni kwamba tu yanamfaa ibilisi, kunifanya ki—kibaraka, kunitupatupa huku na huku, labda kuwa mwanasesere wa kuangaliwa na mtu fulani, labda kuwa mwanasesere wa kuangaliwa na mwanamume fulani, labda sanamu ya mwanamke fulani. Mungu, nifanye mtumishi Wako.” Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao.

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na mioyo yetu.

Naweza kumsikia Mwokozi wangu . . .

Kwa unyofu, mpendwa. Huenda ikawa ni wakati wako wa mwisho. Je! unaweza kusikia hiyo Sauti ndogo?

. . . akiita

Ninaweza . . .

Yeye anaita nini . . . Ni nini kinakuita, kama Mwokozi wako anakuita? Neno.

. . . Mwokozi akiita,

Unapaswa kufanya nini? Kuukana ulimwengu.

Na kuutwaa msalaba wangu na kufuata,
kufuata . . .

“Nimepuuza ubatizo katika Jina la Yesu, Bwana.”

Nitaambatana Naye bustanini,
Nitaambatana . . .

Pamoja Naye, wapi? Kupitia majini, kupitia bustanini, kupitia mahali popote; nyumba ya maombi, kwenye kidimbwi, popote. Amua!

. . . nitaambatana Naye kupitia bustanini
Nitaambatana Naye, Naye kote njiani.

Nitaambatana Naye hukumuni (kama Neno ni
kweli au kama kanisa ndilo kweli),
Nita- . . .

“Iwapo niko sahihi, au Yeye yuko sahihi. Je! dhamiri yangu iko sawa au je! Neno Lake ni sawa?” Uko hukumuni sasa. “Yale nimeamini, je! ni kweli, au Neno Lake ni kweli? Je! ninafikiri ni sawa kuwa na nywele fupi, kuvaa kaptura? Je! ninafikiri ni sawa kuwa mfuasi wa madhehebu?” Je! Yeye alisema nini?

Nitaambatana Naye, Naye kote njiani.

Sasa aniongozako nitafuata,

Nimeinua mikono yangu, pia, Bwana. Bwana, popote pale, je! Ujumbe ujao utahubiriwa wapi? Je! ni hapa nyuma, usiku wa leo, huko Afrika, Ujerumani, Uswisi? Ni wapi, Bwana?

Anio-... (kokote uniongozako, Bwana)...

mimi nitafuata,

Nitaambatana Naye, Naye kote njiani.

Sasa vichwa vyenu vikiwa vimeinamishwa.

²³⁰ Je! utaambatana Naye kila mahali anakokuongoza? Je! utaambatana Naye wakati nyakati ni mbaya, watu wanakutesa, wanakucheka, wanakudhihaki? “Ningali nitakuwa pamoja Naye. Ningali nitaenda. Nitaambatana moja kwa moja pamoja na Wewe, Bwana, popote ulipo. Ningali nitasimama nikiwa mwaminifu na mkweli. Katika vita vikali, ningali nitadumu mwaminifu na mkweli. Kama nikianguka, utaniinua tena, Bwana. “Yeye anayepoteza uhai wake kwa ajili Yangu ataupata.”

Kwa hiyo nitaambatana Naye, Naye kote...

²³¹ Sasa wote mnaomaanisha jambo hilo, kutoka moyoni mwenu, hebu tuinue mikono yetu sasa, na mioyo yetu, Kwake.

Mimi... Aniongozako nitafuata,

Aniongozako nitafuata,

Aniongozako nitafuata,

Nitaambatana Naye, Naye kote njiani.

Atanipa neema na utukufu,

Atanipa...

Bwana Yesu, pulizia lesa hizi sasa. Waponye wagonjwa hawa na wanaoteseka, Bwana. Tujalie, Bwana. Wape uponyaji, Bwana, katika Jina la Yesu.

Na uambatane nami, nami kote njiani.

²³² Mnajisikia vizuri sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Unajisikia yote yako tayari sasa? [“Amina.”] Kama Yeye...

Baragumu ya Bwana Italia, na hakutakuwa na wakati baada ya hayo, (hiyo ni ile Baragumu ya mwisho, sasa)

Na wakati asubuhi itakapopambazuka angavu na nzuri.

Hebu na tuimbe, sisi sote sasa. “Baragumu Yake Bwana wakati ikipigwa.” Tupeni sauti.

Baragumu Yake Bwana wakati ikipigwa, Na siku ya milele ikifika;

Hapo waliokombolewa watakusanyika,

Nitakuwako, jina kuitika.

Na majina yaitwapo,
Na majina yaitwapo,
Na majina yaitwapo,
Kuitika jina nitakuwapo.

Wafu wa Kristo wafufukapo kwa siku ile,
Tutashiriki na fahari Yake;
Waliochaguliwa watakaribishwa Kwake,
Nitakuwako jina kuitika.

Na majina yaitwapo,
Na majina yaitwapo,
Na majina yaitwapo,
Kuitika jina nitakuwapo.

²³³ Na tuinue mikono yetu, tuseme, “Kwa neema Yako, Bwana.”
Kwa neema Yako, Bwana! [Kusanyiko, “Kwa neema Yako,
Bwana.”—Mh.]

Sasa, sisi ni ndugu na dada katika Kristo. Hebu tu tugeuke
na kupeana mikono na mtu fulani karibu yako, na useme, “Kwa
msaada wa Mungu, majina yaitwapo huko ng’ambo!”

Na majina yaitwapo,
Na majina yaitwapo,
Na majina yaitwapo,
Kuitika jina nitakuwapo.

Tunangojea kitu gani?

Baragumu (ile ya mwisho)...Bwana wakati
ikipigwa,
(Tumeshaingia katika Umilele, “Katika
kufumba, na kufumbua jicho.”)... ikifika;
Na basi hapo waliokombolewa watakusanyika,
Nitakuwako, jina kuitika.

Hebu na tuuimbe kwa nguvu kabisa!

Na majina yaitwapo,
Na majina yaitwapo,
Na majina yaitwapo,
Kuitika jina nitakuwapo.

²³⁴ Loo, huo si utakuwa ni wakati wa ajabu! Kutembea tu, siku
moja, na huyu hapa mtu fulani anatokea. “Ni nani? Mama!”
Amina! “Haitachukua muda mrefu sasa.” Katika dakika chache
tu, umebadilishwa. Nasi tutaninii...tutakutana nao, ndipo
tunyakuliwe pamoja nao, kumlaki Bwana hewani. Loo, katika
dakika moja, katika kufumba na kufumbua macho. Unasema,
“Huyu hapa Ndugu Seward, maskini yule ndugu aliyekuwa
hapa kanisani! Aa, huyu hapa Ndugu DeArk. Huyu hapa Ndugu
Nani-...Mbona, angalia hapa, wote wako wananizunguka!
Kuna nini? Hapa katika dakika chache tu...Ninajua tayari
wamenitokea. Haitachukua muda mrefu sasa. Nitabadilishwa
sasa, katika muda mfupi sana, kitambo kidogo tu.” Loo,

naam! Na hiyo asubuhi itapambazuka Milele, angavu na nzuri. Mawingu yote ya ajabuajabu. . .

²³⁵ Kama alivyosema, “Israeli, umekuwa kama wingu la asubuhi, mvuke, na haki yako inafifia.” Na wakati yote yatakapofifia yaingie katika Nuru ya Mwana Ambaye anavishikilia vyote, amina, basi, “Majina yataitwa huko ng’ambo, nitakuwapo.” Vema.

Mpaka usiku wa leo:

Hata twonane huko juu! Hata twonane huko juu!

Hatujui haya yatatukia wakati gani, wapendwa. Imekuwa ni hadithi, kwa muda mrefu, bali ni Kweli, na itatukia. Tuko papo hapo kwenye wakati huo sasa.

Hata—hata twonane huko juu, hata. . .

Kwa neema ya Mungu, tunatumaini, kwenye saa moja na nusu usiku huu.

Mungu awe nanyi daima.

Na tusimame sasa kwa miguu yetu.

²³⁶ Loo, si ni ajabu? “Huu ni ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu.” Tusingebadilisha hii na chochote kile. Mnajua jinsi ninavyopenda kuvua samaki na jinsi ninavyopenda kuwinda, maana ninamwona Mungu huko nje nyikani. Ninapenda jambo hilo. Lakini, loo, nisingeweza kubadilisha dakika moja kwa jambo hili, kwa matukio yote ya mamia ya miaka. Dakika moja ya jambo hili, hiyo ni ridhaa!

²³⁷ Mungu, umba ufufuo ndani yangu! Jalia niwe huo ufufuo. Jalia kila mmoja wetu awe huo ufufuo, ufufuo ndani yangu. Nifanye mimi, Bwana, nipate njaa, nifanye nione kiu. Umba ndani yangu, Bwana, kile ambacho kinahitajika ndani yangu. Nijalie, tangu saa hii na kuendelea, niwe wako; mtumishi aliyewekwa wakfu zaidi, mtumishi bora, aliyebarikiwa zaidi na Wewe; mwenye uwezo zaidi, mnyenyekevu zaidi, mwema zaidi, mwenye kupenda kufanya kazi zaidi; mwenye kuangalia zaidi mambo ambayo ni ya kweli, na kusahau mambo yaliyo nyuma, na mambo yasiyo ya kujenga. Jalia nikaze mwendo kuelekea kwenye mede ya wito mkuu wa Kristo. Amina.

Hiyo ndiyo shauku yetu, sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Vema, hebu, hata tutakapoonana usiku wa leo, hebu na tuchukue Jina la Yesu sasa, kila mmoja wetu sasa.

Peleka—peleka Jina la Yesu,
Ko kote uendako;
Litafurahisha moyo,
Peleka uendako.

Thamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu.

Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

Peleka Jina la Yesu,
Liwe silaha yako;
Utakapojaribiwa . . .



KUTAMBUA SIKU YAKO NA UJUMBE WAKE SWA64-0726M

(Recognizing Your Day And Its Message)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 26 Julai, 1964, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2010 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org